

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report Of**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL OF**

**RIFT VALLEY PROVINCE – BARINGO NORTH AT KABARTONJO  
CHIEF’S OFFICE**

**ON**

**16<sup>th</sup> October 2002**

**DISSEMINATION REPORT & DRAFT BILL, BARINGO NORTH CONSTITUENCY, HELD AT  
KABARTONJO CHIEF'S OFFICE ON 16/10/02**

**Comm. Present:**

Isaac Lenaola

**Secretariat Present:**

1. Robert Gitonga - Asst. Programme Officer
2. Emma Kamunga - Verbatim recorder.
3. Elijah Loiero - District Coordinator

The meeting started at 11.00 am

**Elijah Loiero:** --- ili Draft Constitution ambaye Commission ikisha tayarishwa, pamoja na Report ya Commission, na pia report ya Baringo North Constituency. Kwa hivyo, tunaanza mkutano wetu wakati huu. Kama bado uko nje tafadhali uje karibu, sababu nita mpea Commissioner nafasi hii inaendelea kwa muda mfupi sasa hivi. Kwa hivyo mashughuli yetu ya leo kua hapa ni kujadili tuliowaahidi kwamba, ma-commissioners wakienda kuandika Draft Constitution kwa kutumia maoni yetu, wata rudi huku kwetu ili watupee nafasi ya kuangalia hio Draft Constitution na ku jadili na kutoa maoni, ili iwe ya kwamba hiyo kazi ni ya wananchi wa Baringo North.

Kwa hivyo, leo tumekuja kufanya kazi hio, na bila kupoteza muda murefu ningependa tuanze kwa maombi, halafu baada ya hayo, tufanye introduction ya Commissioner kwa sababu ako hapa, halafu tupatie nafasi Commissioner aendelee. Kwa hivyo,

ninaomba mzee mmoja au mama mmoja ato moto kwa maombi.

**Prayer:** Na tuombe. Mungu wetu, Muumba wetu, Mlinzi wetu, tunakushukuru sana kwa sababu umelinda Commissioner wetu pamoja na watu wake ambao wameandamana naye mpaka wame wasili hapa headquarter ya Baringo North, na umetuleta sisi wengine ambao tumeweza kutana pamoja sasa. Baba tunakuomba kwa unyenyekevu kwamba wale ambao bado watakuja kuungana pamoja nasi kwa ajili ya siku hii muhimu sana ya sheria ya nchi hii ambao itatulinda sisi wote na mali yetu na vitu vyote, tunakuomba uwe pamoja nasi, tangu mwanzo mpaka mwisho wa mkutano huu, ili shukrani zote na utukufu irudi kwako kwa maana ninaomba nikimuamini katika jina la Yesu, aliye Bwana Muombezi wetu – Amin.

**Elijah Loiero:** Asante sana kwa kutukaribisha kwa maombi, sasa tunafanya introduction kwa Committee members wa hii forum ya Baringo North Constituency. Ninge waomba wakaribie kidogo, wale Committee Members ambao wako hapa, kutoka pande ile ili muweze kuji-introduce kwa Commissioner na wageni wengine.

So, pia wale delegates wetu wa Conference, wenye wako hapa wakaribie, ili pia tuwafanyie introduction. So kwa upande huu wangu wa kulia ni Bwana Harun Loyeta, ambaye ndiye Chairman wa Baringo North Constituency Constitutional Committee, yeye ndiyo Chairman wa Committee hiyo, anafanya kazi mzuri sana, baada yake ni Bwana Chelal, ningeomba hawa members wa delegates wote wa kuenda Conference waje hapa mara moja tufanye introduction. Halafu next to Bwana Loite Chairman ni Bwana Chalal, ambaye pia ni member, ametusaidia sana especially kew upande huu wa Iten baada ya Bwana Chalal ni Bwana Barmoso ambaye ametusaidia sana katika hii eneo ya Kipsaraman. Amefanya kazi mzuri sana wa ku mobilize wananchi wa Kipsaraman. Pia ametusaidia sana kwa mashisha - na kuhakikisha kwamba mkutano zetu zote zime faulu. Hapo baada yake ni Bwana Naftali Chelagat, ambaye ni mwakilishi wetu katika Conference ya kujadili mambo ya Katiba, yaani, National Constitutional Conference, ambaye itafanyika mwisho wa mwaka huu, na yeye ndiye amechaguliwa na ma-councillors wetu kulingana na sheria za Acts zile ambazo zinatumiya, kwa hivyo watu wa North Baringo wako na bahati kwa kuwa na Bwana Naftali akiwakilisha District yetu yote ya Baringo.

Yeye pia amefanya kazi ngumu kwa upande wa Civic education. Ame-mobilize watu wengi sana, amefundisha watu wengi ameingia ma-corner zote za District hii yetu, na sana hasa katika constituency hii yetu ya Baring North. Pale pia namuona Mariamu Leksemua, yeye ndio mama ambaye amechaguliwa kuakilisha District yetu katika hiyo Conference ya kujadili Katiba, yeye ni wa kutoka upande wa Marigat, kutoka Jesthu Community, na ni furaha kwetu kuona ya kwamba hata ma Councillors wameona kuna haja ya kuweka kila mtu katika hio delegate list kutoka Baringo District, kwa hivyo anaitwa Mariamu ndio huyo.

Kwa upande wangu wa kulia ni Bwana Kalale Erick, ambaye ni Committee member, yeye ni wa kutoka upande wa Kalabasa, upande wa extreme north wa North Baringo Constituency. Amefanya kazi mzuri sana kwa upande wa civic education, na

ninashukuru yeye kwa sababu ya kazi mzuri. Halafu huyu anaye kuja ni member ambaye pia ni active sana anaitwa Lungurati, yani Jo Chesaro, amesaidia sana kwa kazi ya mobilization na civic education, hasa katika eneo hili la Kabartonjo area, amefanya kazi mzuri, na hata pia kwa upande wa kukutana na wakubwa wetu, wakubwa wa hii Constituency katika mambo mbali mbali za serikali, amefanya hio connection.

Bwana Commissioner ningependa kusema jambo moja ambalo ni muhimu sana kuhusu hii Committee. Committee ya North Baringo imeweza kufanya kazi mzuri kwa Civic education mobilization, hivi kwamba waliweza kufanya fund Raising yao wenyewe kufikia ndimu zao na hivyo wakapata shilling 150,000 ya kufanya mobilization from various people including Mheshimiwa Kiptor, pia tukona Mheshimiwa Kamuren, na pia Mr. Kumen. Walitusaidia kwa hali na pia kwa mali. I believe it is the only Committee that was able to fund Raise.

Kwa hayo ningependa tuwape makofi. So, kwa Baringo generally yote, district mzima Committee hii ndiyo ilikuwa very active, na ndiyo tumepata mobilization, tumefikia watu wengi sana kwa kumobilize. Kwa hivyo kwa niaba ya Commission ninashukuru nyinyi wogte sana. Asanteni. Kwa hivyo nafasi hii, bila kupereka wakati sana ninafikiri nitapea Commissioner Isaac Lenaola, nimewambia kwamba yeye ni mmoja wa Ma-Commissioners kutoka Rift Valley, ni wa kutoka Samburu District. Makomishonas ambao tuko nao ni Bwana Keriako Tobiko, Dr. Mosonic ambaye alikuwako hapa wakati moja, na Alice Yano. Wao ndio ma-Commissioners wetu wa Rift Valley, na tuna bahati kuwa na Bwana Lenaola pia akiwa mtu wa kutoka kwetu. Kwa hivyo ana elewa shida zetu, anaelewa yale yote ambayo tunafikiria maoni wetu. Kwa hivyo nafasi hii ninapatia Bwana Lenaola aendelee na yale ambao ametuletea kutoka Commission.

**Com. Isaac Lenaola:** Asante sana Bwana Coordinator, Wanakamati, na watu wa Kabartonjo, hamujambo? Jambo la kwanza ningependa kuwajulisha wale ambao nilikuja nao kutoka Tume.

Wa kwanza ni huyo kijana mwenye macho manne kama yangu Robert Gitonga, yeye ni mtu wa ku record mambo tukiyazungumza hapa leo, kwa kalamu na karatasi. Tuko na Emma Kaaga, atakuwa akirecord kutumia hiki chombo cha kunasa sauti.

Jambo la pili, ningependa kutoa shukrani za mwenye kiti wa Tume na wana Tume wenzangu kwa hii kamati yenu. Nimesikia kwamba nyinyi ndio Kamati peke yake Kenya ambayo ilitoa fedha zake kwa kazi hii ya Katiba, mjipigie makofi tena. Jambo la pili, mtatueleza kama kuna maswali, kama kuna tashishi kama kuna mambo ambao hamuyapendi, na mambo ambao mnayapenda. Na hivi leo pia niko na furaha kuwaleteeni na kuzungumza nanyi kuhusu hii Katiba mpya ambao ni ya Draft, na hio Draft ndio hii hapa. Wengine wenu mko nayo, na tutatumia leo kuzungumzia mambo ambao iko ndani yake.

Jambo lingine, mulituambia kwamba mungependa kwamba yale mambo mumezazungumzia katika Garbatonjo, katika Baringo North Constituency muje mtueleze kama mumeandika kwa Katiba ama hamukuandika. Na kama hamukuandika ni kwa sababu gani? Kwa hivyo kazi yangu leo ni kufanya hio. Nitatumia hii report yenu ya Baringo North, na kuambieni vile

mulisema hapa hapa, na vile hayo mambo yameingia katika Katiba mpya. Baaada ya hapo, nitawapa nafasi. Mtu akiwa na swali uko na huru na haki kuuliza hilo swali.

Ukiwa kuna jambo ambalo ungependa kuongezea kwa hii Katiba, uko na haki kuongezea hilo jambo. Ikiwa kuna jambo ungetaka kutoa kwa hii Katiba, uko na haki kutoa hilo jambo. Maanake hii si Bibilia kwamba kwamba imeandikwa haiwezi ondolewa ama kuongezwa, ama kuran pia. Hii inaweza kutolewa na kuongezwa. Baada ya hapo, nitawaelezeni kutoka hapa programme ya Tume ni ipi, na tutaenda wapi? Kwa hivyo nikianzilia, wale ambao muko na hii Draft, mtanisaidia kusoma, wale ambao hamna, nitawaelezeni kwa kutafsiri kwa Kiingereza mpaka Kiswahili. Na mptaniwia radhi ninge penda ku zungumza kwa Kiswahili zaidi, kwa hivyo, kama kuna mtu ambaye angependa kuzungumza ki-tugen, utaniwia radhi maanake utazungumza ukipenda lakini ni Kiswahili ambacho kita eleweka.

Jambo la kwanza mulisema kwamba munge penda Katiba ya Kenya iwe na utangulizi. Jambo la kufungua Katiba, kwa maana kila kitabu kiko ina utangulizi. Na Katiba ya sasa ya Kenya haina utangulizi. Na utangulizi mnajua kwa civic education kwamba inatueleza kama wa Kenya sisi ni nani, Kenya ni nini, maanake Kenya si mchanga, na si map, Kenya iko na vitu mingi ndani yake, kwa hivyo wale ambao mukona hii Draft, nitawapeleka katika page number 2. page number 2 iko na Preamble ama utangulizi. Page ya pili, na ina sema hivi. Utangulizi, *sisi watu wa Kenya*, kwa hivyo hii Katiba inatengezwa na watu wa Kenya, haitengezwi na Tume, haitengezwi na Bunge. Hii ni sheria ya kwanza kwa historia ya Kenya ambayo watu wa Kenya ndio wenye kutengeza hiyo sheria. Kwa hivyo inasema kwamba, sisi watu wa Kenya ndiyo wenye kutunga sheria.

Jambo la pili mulisema watu wa Baringo North, ni kwamba mungependa kwa Kiingereza, *the Preamble should acknowledge the country's ethnic diversities and unity of purpose*. Kwamba mungependa hii Katiba ijue kwamba Kenya iko na makabila. Na kwa hio Katiba hayo mambo ya kuwa makabila mengi izungumziwe tujuwe kwamba sisi si watu ijapokuwa sisi ni watu makabila mengi tuko na umoja katika nchi. Na mkiangalia hio Preamble inasema hivi, *aware of our ethnic cultural and religious diversities and determined to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation*. Nyinyi watu wa Baringo North mulituambia hivyo hivyo, kwamba musema hivi, kwamba Kenya iko na mila tofauti. Kenya iko na makabila tofauti, lakini Tumekubali kuungana chini ya nchi moja yaitwa Kenya kwa umoja ya hio nchi. Kwa hivyo mulituambia tuseme hivyo, na mnaona kwamba tumesema hivyo hivyo ka hii Katiba.

Jambo la pili, mulisema kwamba mulipenda kwamba wananchi wa Kenya ndiyo watakuwa na nguvu zaidi katika hii sheria. Wakati mwingine anasikia ni Bunge iko na nguvu, wakati mwingine unasikia ni Rais ako na nguvu, wakati mwingine unasikia ni kotini iko na nguvu, lakini mlisema hivi, mungependa kwamba watu wa Kenya ndio watakuwa na nguvu zaidi katika nchi. Watu wa Kenya. Kwa hivyo page number 4, wale wako na hii Draft page 4, article 1 inasema hivi, *all sovereign authority belongs to the people of Kenya, and may be acted only in accordance with the Constitution*.

Nguvu zote za nchi zitoke kwa watu wa Kenya kupitia Katiba hii yao. maanake Katiba ni yao. na Katiba ndio hupea watu

nguvu, za kutumika katika serikali. na tunasema kwamba hizo nguvu za watu wa Kenya zitoke katika hii Katiba si mahala pengine. Jambo lingine muka sema hivi kila m-Kenya awe chini ya Katiba, iwe ni nani, ama nai, sheria kuu ya nchi iwe juu ya kila m-Kenya. Kwa hivyo article number 2 inasema, The Constitution is the supreme law and binds all authorities and institutions throughout the republic. Katiba ndiyo sheria kuu katika nchi na kila m-Kenya ako chini ya hio Katiba.

Jambo lingine ambalo mlisema ni hili, mungependa mambo ya maendeleo iwe sawa katika nchi nzima, maanake sasa kuna Wilaya zingine ambazo kwa sababu mambo ya historia, Wazungu walikuja mbele huko mashule yakaingia huko mbele hali ya ardhi yao ni mbele, maendeleo hayo ni ya mbele, kuna Wilaya ambazo maendeleo yao ni ya mbele sana. Na kuna Wilaya zingine ambazo maendeleo yake ni ya chini sana. Na watu husema kwamba Baringo District kwa vile wamekuwa na President for 24 years, maendeleo yao ni ya mbele sana. Hiyo si kweli, maanake ukienda Baringo East, maendeleo yao si sawa na Kiambu, ama si kweli, ama ukienda Marigat maendeleo yake si sawa ni Muranga.

Kwa hivyo kuna Wilaya ambazo maendeleo yao si ya mbele kama ya zingine. Na mkasema kwamba Katiba hii mpya isema kwamba, vilaya vyote vijaribu kuwa sawa kimaendeleo. Na zile ambazo hazina maendeleo zipewe nafasi yakuwa na maendeleo kulingana na mambo yao ya kikwao. Kwa hivyo nitawapeleka kwa page number 5, article 14, 15, inasema hivi, the republic shall promote equitable development, recognized and enhance the role of science and technology, eliminate disparities in development between regions of the country. Kwamba hii Katiba, ipewe serikali jukumu ya kuona kwamba tofauti kwa maendeleo kati ya Wilaya iondolewe ili kwamba ili kwa ba kila Wilaya ijaribu iwe na usawa wa maendeleo katika nchi. Na article 18, at least once every year, the President shall report to Parliament and the nation on the measures taken and the progress achieved. Rais wa nchi kwa hii Katiba, ni lazima kila mwaka aende Bunge akawaambia wana Bunge maanake ni wakilishi wetu, awaeleze maendeleo ya nchi imefanyika namna gani? Mbona kuna kuna Wilaya ziko nyuma na zingine ziko mbele, mbona kuna Wilaya ziko mbele sana, wengine ziko nyuma sana, mbona Wilaya zingine mahindi zimekuwa nyingi mpaka inatupwa, na Turkana wanakufa njaa? Tumesema kwamba Rais wa nchi ako na jukumu kueleza kwa nini maendeleo ya nchi haiko sawa Wilaya kwa Wilaya?

Jambo lingine ambalo mulizungumzia Katika constituency hii ya Baringo ilikuwa ni mambo ya vyama vya kisiasa. Mulisema hivi, vyama vya kisiasa vime kuwa nyingi sana Kenya. Saa hizi tukizungumza, kuna vyama 48, kwa sababu gani? Kwa sababu sheria ya kufungua chama cha ki siasa ni rahisi sana. Ni kama kufungua club ya dart, ni kitu rahisi zaidi. Kwa hivyo wewe ukisha kutafuta pesa kidogo unafungua chama na brief case yako unaongoja mwenye kuja kununua siku moja upate fedha. Lakini katika sheria vyama vya ki siasa nui mbinu kubwa sasa ya kuleta democracia katika nchi. Na mkasema kwamba munge penda hivi vyama viwe na sheria kuona kwamba hazifunguliwi, hazitolewi tu ki holela holela. Kwa hivyo article number 87 page number 12, inazungumza juu ya vyama za ki siasa. Lakini tukaona hivi, hatuwezi kusema kwamba kuna haki ya watu kukutana na hatujui mambo yao, halafu tena tufunge vyama vya ki siasa. Kwa hivyo tumesema kwamba kila mtu ako na haki ya kutoa chama chake cha kisiasa. Lakini kuna masharti fulani, ambayo vyama lazima viambatane nayo.

Kwa hivyo ikiona kwamba katika page number 13, article number 90, Tumesema kwamba the Electoral Commission shall not register a political party if that party is found to be purely on religious linguistic racial, ethnic sect, corporatist, regional basis and so on. Hatupendi vyama vya siasa ambavyo ni ya kabila moja, ama ni ya wanawake pekeyao, ama ni wanaume pekeyao, ama ni ya Kanisa ya IAC pekeyake ifungue chama yake. Tungekuwa na chama ambacho ni chama cha kitaifa. Mimi nikifungua chama yangu sasa niite chama changu na pesa, haitakuwa tena chama cha wananchi. Ama chama cha akina mama wazee pekeyao, ama chama cha ma-councillor pekeyao, ama chama cha watu wa Kabartonjo pekeyao, haitakuwa chama tena. Kwa hivyo kuna sheria kali ni kuhusu vile unge fajilisha chama vyama vya kisiasa.

Pia mkasema kwamba mungependa vya viwe na fedha fulani kusaidia mambo yao ya ku-mobilize watu wao, na kufunza watu mambo ya haki zao, na democracia yao. kwa hivyo katika hi Katiba Draft tukona sections kuhusu mambo ya fedha kwa party.

Lakini party haikubaliwi hasa kutumia pesa kwa kwa ajili ya kulipa watu mishahara, ama kulipa watu mazawadi, hapana. Kwa hivyo huwezi kufungua party yako hapa ukafanya bibi yako secretary mtoto wako treasurer, members ni watu wa familia yako, ndio upate pesa kutoka kwa serikali ya kulipa mishahara ya nyumba yako.

Tumefunga hiyo laini, hiyo mfereji yakula fedha ya chama cha kisiasa. Kwa hivyo huwezi kufungua chama yako hapa ukafanye chama cha watu wa Kabartonjo, ndio mpewe pesa mkule peke yenu Kabartonjo, hapana. Kwa hivyo ni strict system ya registration na pia kutumia fedha katika chama.

Nikisonga mbele, mlizungumuzia sana juu ya Bunge. Mambo ya Bunge mlisema sana sana sana hapa. Na jambo kubwa mlisema hapa ni kwamba munge penda kuwa na nafasi kabla ya miaka mitano kwisha, kama Mjumbe hafanyi kazi ya ujumbe, munge penda miaka mitano kabla miaka mitano kwisha huyo Mjumbe arudishwe nyumbani na mwingine apigiwe kura. Kwa hivyo ukiangalia article number 112 katika page ya 15 Tumesema hivi; A member referred to in clause 1 may be recalled from that office on any of the following ground:-

- a. physical or mental incapacity that renders the member incapable of performing the functions of the office. Katika Bunge la sasa, kuna Wajumbe wawili ambao ni wagonjwa kabisa miaka mingapi, tatu. Si makosa yao kuwa wagonjwa. Lakini ikiwa Mjumbe hatoki kitandani, ako hospitali kila siku, inge kuwa sawa kwamba akae akala mishahara na kazi yake ya ujumbe haifanywi na mtu mwingine. Maanake hatuna Mjumbe Assistant; kuna Assistant katika -----? Kwa hivyo mwingine akiwa mgonjwa huwezi kusema kwamba assistant afanye kazi ya MP. Tukasema kwamba Mbunge akiwa mgonjwa mpaka afanye kazi ya ujumbe, basi arudishwe nyumbani, na mwingine ateuliwe, maanake si makosa yake, lakini si pia makosa ya watu wa constituency wasikuwe na mjumbe katika Bunge.
- b. Misconduct likely to bring hatred ridicule contempt or discredit to the office. Ikiwa mjumbe ni mtu wa haibu, mlevi mlevi barabarani matusi matusi ka mkutano, ile heshima ya kiongozi anakosa. Tukasema kwamba sisi mjumbe kama huyo mko na haki ya kusema kwamba umekosa heshima ya ofisi yako mjumbe njoo nyumbani ukaa na sisi kunywa changaa' kunywa muratina kwa maana hiyo sio ofisi ya watu wa muratina na changaa'.

c. Jambo la tatu, persistence desertion of electorate without reasonable cause. Ikiwa mjumbe haonekani katika constituency, haonekani katika Bunge, haonekani kwake nyumbani, hana ofisi kwa constituency basa hana sababu ya kuwa mjumbe. Mjumbe mwenye kutoro, mwenye kuhepa watu hana sababu ya kuwa mjumbe tena. Na jana Kabarnet nika wapa watu wa Kabarnet mfano mzuri sana. Mwaka ya 80, katika Moyale Constituency, kukaja mzee mmoja fulani, hii ni story ya kweli si ya kutilia, ni ya kweli. Akaja huyu Mjumbe akasema hivi, mkinipigia kura nitafanya hivi, nitafanya kile, mashule itakuja tele hapa, maji itajaa hapa, barabara itatia lami mara kumi, watu wakaona huyu ni mtu wa maendeleo. Na mjumbe ni mtu wa nini, wa maendeleo.

Kama huna maendeleo, huna haja kuwa mjumbe. Huyu jamaa wangu sasa alipopigiwa kura akaambia watu basi ninaenda Nairobi bye-bye. Wakafikiri ni bye-bye ya kwenda na kurudi. Kumbeni ni bye bye ya kwaheri kabisa. Hajaonekana miaka ngapi—family yake akahamisha akapeleka Mombasa. Akafungua company ya Clearing and Forwarding Mombasa. Kazi yake ni Nairobi na wapi, Mombasa. Sasa Moyale iko Mombasa? Moyale iko wapi? Iko huko Eastern Kenya. Hajaonekana miaka mingapi.

Mjumbe kama huyo, ako na sababu useme ni kama Bunge, tukasema katika hii Draft kwamba mjumbe kama huyo, arudishwe nyumbani aambiwe umeshindwa kazi kwenda fanya kazi Clearing na Forwarding Mombasa, wachana na sisi na Mjumbe wetu ambaye tunampenda. Kwa hivyo katika hii, tumesema kwamba wajumbe ambao hawafanyi kazi kwa miaka mitano warudi nyumbani kamble hiomiaka mitano kwisha. Lakini njia ya kufanya hii ni gani? Maanake unajua siasa ya Kenya pia ni kali. Mimi nikiwa nimesimama kwa kuramahali fulani halafu huyu anishinde, siwezi ngoja miaka mitano. Ninge penda kilasiku akuwe wapi, ango'lewe. Kwa hivyo sub-article 3 inasema nini? "The recall of a member of Parliament shall be initiated by a petition in writing signed by at least 30 percent of the voters of the constituency. Ukitaka mjumbe atolewe, kama auko na moyo sana kwamba huyu mjumbe lazima atolewe, nenda katika hiyo constituency, chukua signature ya wapiga kura asili mia thalathini, thirty percent.

Kwa hivyo kama kuna voters 1000,000 kwa constituency, ni ngapi utachukua signatures ya 30,000 voters kwa hio constituency. Pelekea Speaker wa Bunge. Speaker atapelekea Electoral Commission. Commission itakuja kwa constituency, iketi chini, isikie malalamishi ya watu wa hio constituency. Halafu itaamua kama kweli kuna sababu ama ni siasa ya kumalizana.

Kwa sababu pia, hatutaki Mjumbe kutolewa ikuwa ni kazi rahizi tu, unachukua signature 10, nasema huyu mtu ni mtoro, kumbeni hio ni siasa ya kumalizana, anataka kumtoa huyu. Kwa hivyo hii system ni ngumu, na ni rahisi pia. Kwa hivyo kama kuna moyo sana kutaka mjumbe akuje nyumbani, pitia hivyo, isikuwa tu kuandika baruwa halafu Mjumbe anaambiwa kuja nyumbani.

Jambo lingine mulisema hapa, mungependa kuwa na Bunge ilio ya nyumba mbili. Nyumba ya chini Lower House, na Nyumba



ya juu, Upper House. Na Upper House itakuwa nyumba ambayo iko na watu wamekomaa. Si vijana, nyumba ya wazee, kuchunga hawa vijana wa Lower House. Kwa hivyo katika Upper House ukitaka kuwa mjumbe wa Upper House ni sharti uwe na miaka 35 kwenda juu. Ukiwa katika Lower House, nyumba ya chini Parliament kama ya sasa, uwe na miaka 21 kwenda juu. Kwa hivyo kama kuna vijana kwa Lower House, kuna wazee katika Upper House. Na Upper House, kila Wilaya itamchagua Senator ngapi? Moja, kila District, kwa hivyo Baringo mukona one Senator aende Upper House. Lakini hii Lower House, itabaki na wale wajumbe wenye wangapi 3, watatu, Baringo North, Baringo Central, an Baringo East. Kwa hii ya chini, iko na Mps 210, hii ya chini iko na MPs 70. Na katika hii Katiba mtaona kazi ya Upper House ni gani na kazi ya Lower House ni gani?

Jambo lingine mlisema, hii mishahara wa Bunge hamunge penda wa-Bunge wajipatie mishahara, maanake mnajua kwamba kwa miaka 3 uliopita wajumbe waliongeza mishahara mara ngapi? Mara ya kwanza waliongeza mpaka wanakula 800,000 kila mmoja. Ma Ministers wanakula million moja kila mwezi. Mara ya pili wakajipatia insurance ya afya kila mjumbe insurance ya million 10. Mara ya tatu wakajipatia ile housing loans ya million kumi. Na hawakuuliza mtu yoyote kwamba hii mishahara tutatoa wapi.

Walikuja hapa akawauliza kwamba tuongeze mishahara? Na unajua mimi ninajua kwamba ukiandikwa kazi huwezi kujiandikisha mishahara pia. Mwenye kukuandika anafanya nini, anakupa mishahara. Na waBunge nani anawandika hawa kazi? Kwa hivyo ingekuwa vizuri; kabla hawaja ongeza mishahara, wange tumia Tume kidogo yazunguka kusema je tukiona kazi kubwa kama waBunge kweli, tunasafiri sana kwa constituencies kweli, tunafanya harambee sana kwa constituencies kweli, tungependa sana mtupatie mishahara kiwango fulani ili maharambee tulipe tupitie ninyi kuwaona nyinyi, halafu pai sisi tunahesabu tuseme kwamba kwa hesabu yetu upewe mishahara fulani.

Lakini hamwezi kukaa chini kwa Bunge, na siku hiyo by the way, walikuwa wakipanga hii mishahara, mambo ya vyama ikapotea. Hakuna ati wewe ni KANU, wewe ni mtu ya DP, wewe ni mtu ya sijui SDP, ilipitishwa unanimously. Kila mtu kwa Bunge alikubali. Mambo ya vyama yalipotea siku hiyo, kwa sababu ni nini, ni mishahara yao. Tukasema hivi, article 21, page number 15. A member of Parliament shall be paid such salaries, allowances and benefits as may be determined by the Salaries and Remuneration Commission. Tumefungua Tume Special, kazi yake ni kutunga mishahara ya wakubwa wakubwa hao. Ili kwamba wakitaka kujua mishahara ya MP waaje kwetu watuulize. Wasikae chini wakashau vyama, wakaambiwe kwamba mishahara zao sasa itakuwa mishahara fulani.

Jambo lingine mlisema hapa Baringo North, unaona mimi ninazungumza kufuatilia report yenu. Sio mambo hamkusema, haya mambo si yangu, ninafuata report yenu na kuangalia mambo katika hii Katiba. Kasema hivi tena, mungependa kwamba Bunge liizinishe appointment hizi kubwa kubwa, kwamba President akimteua mtu, wacha Bunge ipitishwe huo uteuzi. Sababu gani, mlipenda kwamba watu wakiteuliwa waakilishi yenu pia wajue kwamba hawa watu wanafaa kwa hizo kazi. Kwa hivyo katika article number 103, inasema approval of appointment by Parliament. Na maofisi kama gani Tumesema Parliament approve?

Ofisi ya Prime Minister. Wacha President ateu Prime Minister na Parliament approve. Wacha President, wacha; Parliament approve. Wacha President appoint Ambassadors, lakini Parliament I approve. Governor ya Central Bank akiteuliwa na President, Parliament I approve. Kwa nini tunasema hivyo, ili kwamba watu ambao wako katika maofisi kubwa kubwa, ni watu ambao wanafaa hio kazi.

Jambo lingine ambalo mlisema katika Baringo North kuhusu Bunge; mambo ya majaji, majaji pia President akiwateua, wacha Bunge izinishe kwamba hawa watu ni sawa kuwa majaji. Jambo lingine mlisema hapa ni mambo ya serikali, mungependa serikali ya aina gani. Lakini kabla hatujafika hapo, hebu ni zungumze juu ya ofisi ya President. Mlisema hivi katika Baringo North, “The Constitution should provide that the President shall be subject to the law” kwamba Rais pia awe chini ya sheria. Muka sema hivi, “The Constitution should limit the powers of the President. Katiba itoe nguvu za Rais urudi chini kidogo. Maanake, hata Rais wa sasa amesema kwamba hii Katiba ya sasa inampa yeye kama Rais nguvu nyingi sana. Kwa hivyo hii Katiba inajaribu ku reduce nguvu za Rais, lakini haikumtoa nguvu zote. Kwa hivyo article 148 page 19 ina zungumza juu ya nguvu ya Rais wa nchi. Na ina sema hivi, “The President is the Head of State. Rais katika hii Katiba atakuwa ndiye mkubwa katika nchi. Jambo la pili, Commander in Chief of the Defence Force atakuwa Mkuu wa Majeshi ya Kenya. Na unazungumza tukiita defence force tunakuwa na Armed Forces. Armed ni ile watu wanguvu sana. Lakini hapa tumesema defence maanake kazi yao ni kufanya nini, ku defend sisi, hapa ku harm sisi, ni kuchunga sisi.

Kwa hivyo, Rais ni mkuu wa hawa majeshi wa kuchunga sisi. Tatu, President atakuwa akifungua Bunge, and kuifunga Bunge. President ndiye atakaye appoint Prime Minister. Ndiye atakaye appoint Cabinet. Ndiye atakaye appoint watu wa kisheria, majaji. Ndiye atakaye a sign documents za international kama vile agreements, kama signed agreement ya Somalia jana. Kwa hii Katiba, mambo ya international ni kazi ya Rais wa nchi, si kazi ya Prime Minister. Rais ndiye atakeye sema kutakuwa na vita kati ya Kenya na Somalia, si Prime Minister. Ni yeye atasema kwamba ma Ambassadors watakuwa wameteuliwa.

Kwa hivyo ukiona hapa, nguvu za Rais ni zile zile tu ako nazo sasa. Lakini tumesema kwamba wacha Parliament pia ipate nguvu ya kuizinisha, kama hivyo Tume fanya. Pia Bunge ikipitisha sheria ni kazi ya Rais wa nchi kuweka kidole kwamba iko sheria ya Kenya. Kwa hivyo ukiangalia hii Katiba, mtu akisema kwamba Rais katika hii Katiba hana nguvu, sielewi walisoma Katiba gani, maanake hii imempatia Rais nguvu lakini tumeileta chini kidogo, isikuwe nguvu nyingi sana, mpaka inakuwa overdose ya nguvu.

Na je huyu Prime Minister mnasikia tumesema katika hii Katiba Prime Minister aweko, yeye ni nani? Article 170, The Prime Minister is the leader of the Cabinet and presides at meetings of the Cabinet. Tume gawa nguvu ya Rais mara mbili. Hivi sasa Rais ni mkuu wa nchi na pia mkuu wa serikali. Tume gawa hivi, Rais abaki kuwa mkuu wa nchi, na mkuu wa serikali awe nani, Prime Minister. Na mkuu wa judiciary akuwe nani, Chief jaji, na mkuu wa Parliament atakuwa nani Speaker, lakini hawa wote wako chini ya nani, mkuu wa nchi ambaye ni President.

Halafu jambo lingine, mawaziri: Kwa hii Katiba Draft, Tumesema nini kuhusu mawaziri? Sisi wa-Kenya walituambia hivi, na mkasema nyinyi watu wa Baringo hamkuzungumza juu ya Cabinet, mlisema tu ya kwamba the President should choose the Prime Minister. Hamkuzungumza juu ya Cabinet, kwa hivyo nitawambia vile wa-Kenya wengine wenzenu walisema juu ya Cabinet. Walisema hivi, wacha Mbunge awe Mbunge. Wacha waziri awe waziri. Kwa sababu gani? Kwa sababu, wameona kwamba mtu akiwa waziri na pia akuwe Mbunge, anashika moja anaachilia nyingine.

Kwa mfano, mtu akiwa waziri wa Kigeni, Foreign Affairs, kazi yake nyingi ni ya wapi? Ya nje; kwa hivyo haonekani kwa constituency, haonekani kwa Bunge, haonekani kwa ofisi, maanake kila siku ako wapi, ako Paris, ako London ako New York kila mahali. Kwa hivyo ofisi inaumia, Bunge inaumia, na constituency pia inaumia. Kwa hivyo wa Kenya wakasema hivyo na tukawafuata, wacha Mbunge awe Mbunge full time. Wacha waziri awe waziri full time. Ninasema ukweli sasa, hii mwezi moja uliopita, waziri gani ako ofisi, ni hio ukweli. Wako kwa ofisi, si wana campaign? Na kazi ya ofisi, nani anafanya? Na Bunge wako Bunge? Leo kwa ma-gazetti jana speaker alikuwa anasema hakuna quorum kwa Bunge maanake mawaziri wako wapo, wako kazi ingine ambao pia ni ya maana lakini wange kuwa wanafanya kazi ya Bunge hapana kazi ingine ile ya maana zaidi. Kwa hivyo saa zingine ni vizuri kusema kwamba Bunge na Cabinet ikuwe separate.

Haya nitazungumzia juu ya Provincial Administration, na report yenu ineam kwamba mulisema, mimi sikuwa Baring North, nilikuwa Baringo Central, kuchukua maoni lakini wenzangu walikuwa hapa na mlisema hivi, The Constitution should provide that the Provincial Administration shall be scrapped. Serikali za Wilaya zifanywe nini, ikuwe scrapped. Mukasema. The Constitution should provide that the Chiefs shall be elected. Nani apigiwe kura, ma-Chiefs. Mukasema tena, the Constitution should provide----

Tukasema kutakuwa na serikali ya vyango vinne. Serikali ya ya Sub Location, na iko na kikao cha wazee katika sub-Location. Pili kuwe na serikali ya Location, kuwe na council katika Location. Wa-Kenya wengi wakasema kwamba hawaoni maana ya division, kwa hivyo wakasema serikali iwe katika Wilaya. Mukasema hivi, kuwe na serikali katika Wilaya. Nne, kuwe na serikali ambaye ni nguvu yake ni kidogo katika mukowa, Province, lakini nguvu nyingi iwe wapi, Districts. Kwa sababu gani? Niliona kwamba sometimes, Province ni mbali na pia Nairobi ni mbali na jana Kabarnet niliwapa watu mfano mdogo tu.

Mnajua mahali inaitwa Loitokitok mumesikia hiyomahali, iko Province gani, Rift Valley, Wilaya gani, Kajiado. Lakini iko wapi, border ya Kenya na Tanzania. Halafu DO wa Loitokitok, DC wote wako wapi. Anatoka Loitokitok, anafika Emali, Sultan Hamud, Kajiado, Nairobi, Limuru, Gilgil, aende wapi, Nakuru, maanake serikali yake iko wapi, na District yake iko wapi, Kajiado sio. Unapita Kajiado District unaenda mpaka wapi, Nakuru District maanake Nakuru ndiyo Provincial headquarters. Ama Lokichogio iko Province gani, Wilaya gani, na DO wa Turkana akiwa Lokichogio DC yake iko wapi? Nakuru, kwa hivyo unatoka Lokichogio Lokitaung, Kakuma Lodwar, Kitale Eldoret, Timboroa, Kapsabet ---- mpaka wapi? Nakuru, maanake serikali iko wapi, Nakuru. Na kama Serikali ingekuwa Lodwar si ni karibu zaidi. Kwa hivyo katika hii Draft

Tumesema wacha serikali iwe katika Wilaya kwa sababu ni karibu.

Hakuna maana sasa kwangu kwamba ukitaka passport ama driving license ama road license ama insurance mpaka Nairobi. Hata wale wazee wale wako na short gun ile ya ukoloni license zake iko wapi, Nairobi. Na jee kama hizo vitu vyote vingekuwa Kabarnet, dakika ngapi kutoka hapa Kabartonjo? Unaingia asubuhi, unapewa saa nane una kula jioni kwako nyumbani. Lakini mzee anapelekwa mpaka Nairobi kuchukua road license ya shilingi 1500, ukifika huko unaambiwa arudi Kabartonjo chukua ile ya zamani na ulisahau nyumbani. Huyu mzee tena mpaka wapi, ukifika unaambiwa lete ile ya 2000, wacha ya 2001, rudi tena Kabartonjo.

Tukasema hivi sisi, wacha kilakitu viwe katika Wilaya. Hata pension ya wazee wasifuatilie Nairobi, ifuatiliwe wapi, Kabarnet kwa District. Kwa sababu wazee wakati mwingine unaambiwa file yake iko Nairobi na wanajua file yake inaandikwa Kabartonjo Baringo District. Hio file kuletwe Kabarnet ni ngumu, tukasema hivi kila kitu kiwe katika wapi katika Wilaya. Na je mulisema kwamba hawa watu wakuu wa hizo Locations kwa Wilaya wapigiwe kura.

Maanake mulisema hampendi kwamba mkuu wa Wilaya anatolewa mahali anatolewa hamjui kama ni mtoro ma ni mkora ama ni mlafi ama anapenda kukata forest na analetwa wapi, kwenu. Mkasema wacha mkuu wa Wilaya apigiwe kura na watu wa hio Wilaya. Kwa hivyo sub-article 218(4), "The District administrators is elected directly by the voters of the District." Kama mnataka kuwa na DC wenu kura ni ya nani, yenu. Na kama mnataka kumtoa article 218 sub article 6, inasema kwamba mnaweza kum-dismiss akiwa mtu mlagai, akiwa mtu hafifu, akiwa mtu ambaye hana heshima kwa watu, kwa vile kura ni yenu, na kumweka, pia kura ya kumtoa ni ya nani, ni yenu.

Jambo lingine: mali ya asili ya Wilaya, article 226, District shall be entitled to a substantial share of the national revenue from local resources, and for the Location of a fixed percentage for the communities in those areas the resources are generated. Mali ya Wilaya ibaki kwa wapi, kwa Wilaya. Kwa mfano; ikipatikana gold katika Baringo North, kwa sheria ya sasa hiyo gold ni ya nani? Ni serikali. Iende kwa serikali. Lakini itakuwa aje kwamba mali ya asili ya watu wenye kuishi hapo itolewe wakiangalia iende ikuliwe Nairobi? Tunasema hivi sisi, percentage kubwa ya hiyo mali ya asili ibaki katika wapi? Katika Wilaya.

Pili kuna wato ambao wanaishi mahali hio mali inatoka kwa hiyo Wilaya. wacha wao wapewe percentage pia ya hiyo mali. Kwa mfano mimi ninatoka Samburu. Na huko Samburu kuna lioness inapenda ---simba inapenda hii nyama ingine. Na wazungu wanaingia ndege siku hizi kuja wapi? Kuja Samburu. Na hiyo pesa ikitolewa inaenda wapi? Nairobi, Ministry of Local Government. Halafu sisi tunaongoja iende huko Nairobi izunguke ipite Nakuru ikuja mpaka wapi, mpaka Samburu. Na mnyama hajui kwamba hii ni park ama hii ni shamba la mtu, inajua? Leo iko kwangu kwa shamba, kesho iko wapi? Kwa park. Na mimi silipwi kwa sababu mimi sina park, lakini park inalipwa kwa sababu ni park. Tunasema hivi, watu ambao wako karibu na hio mali hapo wapewe kiwango fulani maanake hawa ndiyo wenye kuchunga hiyo mali.

Jambo lingine katika hii Draft article 222, inasema kwamba:-

- a. Nairobi has the status for the capital territory. Nairobi iwe na mali yake special maanake ni nchi ya mtu fulani. Nairobi haina wenyewe, ama iko na wenyewe? Mimi ninaishi Nairobi na sasa mimi si mtu wa Nairobi, kipande yangu imeandikwa Samburu. Hakuna mwenye Nairobi, tukasema Nairobi ni ya kila mtu. Kwa hivyo tuwe na status yake special.
- b. A city of a municipality has the status of a District. Hakuna mjaluo hapa ama iko jalu moja hapa kutoka Kisumu City, tunasema kwamba ikuwe kama District, Mombasa city ikuwe kama District. Kabarnet ikuwe kama District maanake ni municipality. Towns and urban centres kama Kabartonjo ikuwe kama Location. Iwe na serikali yake ndogo katika hiyo area ya urban centre.

Tuende katika hali ya haki za bin Adam. Kuna haki ambazo watu wako nazo ambazo hatupewi na mtu yoyote. Hatupewi na serikali, hatupewi na kotini. Hizi haki ni haki zetu maanake sisi ni bin adam. Haki tunapewa na nani? Na Mungu. Article 32, every one has the right to life, haki yia kuishi. Kuna mtu amekuwekea katika dunia hii kwamba lazima huishi? Ni ya nani hiyo, haki kama hizo ni haki zetu maanake sisi ni bin adam. Akina mama ambao leo wameingia hapa Tumesema kwamba mila zetu inawafinya sana, mila hazikubali kwamba wanawake wako mahali katika uozi, niliwapa mfano moja katika kabila yetu wa Usamburu, mimi nikiowa mwanamke, from the first day nikipeleka yeye kwetu anatembea wapi, wapi, nyuma sana maanake nani mwenye mambo, mwanamume sio. Mwanamke ako wapi? Na kutoka siku hiyo mpaka siku atakufa ako wapi? Lakini nimesema maanake ni mila imekuwa nyingine, wacha pia wakubaliwe hata hawa haki zao kidogo tu pia hawa wakuwe kama watu.

Kwa hivyo article 35 women have the right to equal treatment with me. Usawa mwanamke na mwanamume, na pia wako na haki zao katika sheria kama wanamume. Halafu article 36, wazee hatujawasau, kwamba wazee wako na haki. Wasisaulike maanake walikuwa wamekomaa, kwamba wamekuwa watu ambao wamekuwa na nywele nyeupe na vipara vipara, wanatembea na miti, pia wako na haki. Kwa hivyo older members of society, have the same rights kwa hii Katiba, kwa hivyo wazee pia tunawakumbuka.

Pia watoto article 37, watoto wako na haki kwa hii sheria. Halafu kuna watu wanapenda ku zaa zaa, kuza.lia watoto wa watu, wasichana wamezaliwa wakiwa form four, kijana anaendelea na masomo, msichana anaendelea na masomo, halafu mtoto hachungwi na huyo kijana, msichana analeta mtoto kwa mama yake achungwe, Tumesema kwamba hiyo tabia mbaya hii Katiba haikubali, kwa hivyo a child's mother and father whether they marry each other or not have an equal duty to protect and provide for the child.

Mtoto akizaliwa, hata kama baba yake na mama yake hawajaowana wote wawili wako na jukumu zaidi ku chungu huyo mtoto.

Kwa hivyo wale watu mnazoe katika Kabartonjo unaenda fulani fulani, kuzalia manyumba ya watu mumekamatwa leo. Haya.

Jambo lingine, “All children whether born within or outside wedlock are equal before the law. Mtoto ambaye amezaliwa ndani ya ndoa ama nje ya ndoa ako na haki sawa kwa hii sheria, Haya. Kwa sababu, mnajua tunaliya sana kwamba watoto wa mitaa wamejaa. Lakini hawa watoto wako na mababa. Hawakuzaliwa na hewa, kuna mtu fulani alimzaa huyo mtoto. Kwa hivyo tunasema kwamba mtoto yoyote awe na haki sawa kwa hii sheria.

Article 38, haki ya kijamii. Haki ya kuowa na kuolewa, haki ya kuwa na jamii yako, na kulitunza tunazo hapa. Halafu kuna watu walemavu ambao pia kwa miaka mingi hukuwaheshimu, hutuwaangalii, watu vipovu, watu ambao hawasikii, wale ambao hawatembezi vizuri, tunasema kwamba pia hao wako na haki katika hii sheria. Na kuanzia hapo hii Tume imetoa hii report yake kwa lugha ambayo inasomwa na wale ambao hawajui ku—hawa oni tumewandikia report hii lya Katiba hii kwa hii lugha ya Braille, wale ambao wako blind. Kwa hivyo pia hao wako na masharti ya kusoma hi lugha yao ya Braille, unaona vile imechapwa na ile mikono. Kwa hivyo sisi tumeenda mbele kidogo, tumewatambua katika hii Katiba mpya.

Halafu mlizungumza sasa juu ya haki ya kuabudu. Mekanisa yamekuwa mengi, sikuhi mtu akiwa broke anafanya nini? Anafungua nini, kanisa ndio tanzwe sema toa ndugu toa dada, lakini njaa ndiyo sasa ---- Article 44 kila mtu ako na haki ya kuabudu, lakini katika report yetu tunasema kwamba registration ya mekanisa ikuwe strict, ili mekanisa ya pesa ikuwe nini, chache. Ma kanisa ya kuabudu sijui shetani ifanye nini itolewe.

Kwa sababu sasa kuna mambo mengi sana, sisi Nairobi Tumeona mambo mengi sana. Na kuna mekanisa ambao kazi yao ni usiku tu. Hawaabudu mchana. Wanaabudu nini? Na hakuna kitu kizuri inafanyika usiku ninawaambia ukweli. Kwa hivyo inaonekana kwamba haya mekanisa ya usiku usiku kwamba wanasema ni ya ajabu tuweke registration yao ikuwe kali ili maajabu na mambo ya haibu na mambo ya siri ya kimungu mungu isifanyike hapa katika Kenya. kwa hivyo let us restrict rules iwe restriction katika mekanisa.

Hapo haki za mila na lugha article 63, kila ako na haki kutumia lugha yake, kutumia mila yake, na mambo kama hayo. Na jambo ambalo tulikuwa na shida sana kuliandika hapa ilikuwa mambo ya kienyeji. Tuliambiwa, kuna mila fulani ambazo hazifanyiki mpaka kuwe na pombe ya kienyeji. Na serikali inasema kwamba hii pombe ya kienyeji si halali. Na kusema hapo kama tukona haki ya kukuwa na mila yetu halafu tunafunga pombe, basi tutakuwa tunajipatia mila nusu. Tuka-suggest sisi kwamba maanake tumepata report kubwa kwamba kuna zile pombe ambazo lazima zikunyiwe kwa heshima ya ceremony fulani ya ki-mila. Kama kwetu ki Samburu huwezi kwenda kuowa kama hujapeleka ile pombe ya asali.

Tena kuowa bila pombe ya asali hiyo inataka mtu ovyo ovyo, si mtu ambo –hauko serious kuowa. Kwa hivyo tumesema kwa report kwamba kuwe na procedure ya ku-licence si pombe ya kimila lakini ceremony ya kimila peke yake. Si ile ya zamani ya ile busaa clubs, tunakunywa pombe mpaka wazee wanakojoa kwa barabara. Hjiyo tumekataa maanake italeti haibu katika nchi. Kwa hivyo mimi ninasikia kuna mambo kama hayo ambayo ni vizuri kufanya lakini kwa kutunza na kufuata mila zetu

maanake sisi ni wa Africa, sisi hapana Wazungu. Na mzee mmoja aliniuliza juzi kwa ini mnasema ati pombe ya Tusker iko na licence na Muratina haina licence? Nikasema maendeleo suit na time ni maendeleo ingine ambao haiku kuwa zamani, lakini tutayangalia katika mambo yanayokuja.

Halafu kuna haki ya kuwa na afya njema. Article 67, article 68, haki ya kuwa na masomo ya bure na ya lazima katika primary school. Kwa hivyo serikali imetoa hiyo jukumu. Si kama sasa at unaambiwa ni ya bure lakini kuna hii shillingi kumi, kuna hii ya 50, kuna hii kitabu, kuna hii pencil, tumesema hapa, serikali iwe na jukumu kisheria kuona kwamba elimu ni ya bure na yalazima. Na serikali isiseme kwamba haina fedha ya kulipa haya mambo, haina sababu yakuwa serikali tena, maanake ni sheria inasema hiyo. Haki ya kuwa na nyumba ya kuishi, haki ya chakula haki ya maji, iko hapo.

Halafu kuna haki ya watu ambao wanafungwa. Unajua siku hizi mtu amechukuliwa na polisi, unawekwa ndani wiki mbili haujulikani mahali uko maanake sheria haikuwi direct kwamba mtu asitiwe ndani kwa muda fulani. Kwa hii Katiba article number 68-ukishikwa na polisi ni sharti uwachiliwe ama uende kotini within 48 hours. Mambo ya kuweka mtu kwa mwezi mzima ama wiki tatu ama wiki mbili tumekataa katika hii Katiba. Halafu kuna jambo kubwa hapa, tunaambiwa kwamba hizi haki ni nzuri na ni safi lakini kuna njia gani ya fuatilia hizi haki ni kwamba nikifanyiwa unyanyazaji na mtu fulani, niko na mahali ya ku complain. Maanake sasa ukiwekwa na polisi ndani ya cell kwa mwezi mzima, ukienda kwa OCS, si OCS ni polisi tu. Ama OCS akikataa kuzungumza na wewe unaenda kwa OCPD, OCPD si ni polisi tu.

Kwa hivyo huwezi kwenda kwa simba kwa complain kwa simba mwingine, maanake simba ni simba. Kwa hivyo kwa hii Katiba tumesema nini? Tumesema kwamba ukona haki ya kwenda katika Tume ya haki za ki bin adam, Human Rights Commission. Kila Wilaya itakuwa na kila kitu Kenya hii, kwa hii Katiba. Ofisi yake itakuwa katika kila Wilaya. Kwa hivyo ukifinywa, kuna ofisi ya kupeleka nini complain hapo. Na hii ofisi inaitwa Ombudsman, mtu ambaye kazi yake ni ku protect sisi, ombudsman, protector of the people, umteteaji wa nani? Wa watu. kwa hivyo DC akikufinya kuna ofisi ya complain., Polisi akikufinya kuna ofisi ya complain.

Pili unaweza kwenda kotini mahali popote na ku-file case kwamba haki zangu zimechukuliwa. Lakini kuna swali hapa, kama hujui sheria na sisi mawakili ni watu wa kulipwa, utafanya nini kama hauna pesa na huelewi sheria? Kuna jibu hapa: kuna mtu anaitwa katika article number 210, page 26, Public defender, wakili wa watu. Unajua sisi ni mawakili wa kulipwa biashara kwa sababu kama mnakuwa na mawakili katika District ambaye halipwe sisi biashara imeenda.

Lakini tunasema hivi, The Public Defender shall provide legal advice to persons who are unable to afford legal services. Kwa hivyo, haki zako zikichukuliwa si lazima uongoje uwakili kama mimi ambaye lazima aseme lete deposit ya kufungua file, lete pesa ya kortini, lete pesa ya ku-bribe jaji, kuna wakili hata hana malipo. Unaona hii Katiba ni tamu sana. Kwa hivyo kama haki zako zinafinywa na mtu fulani, kuna njia hizo mbili za kuona kwamba hizo haki zina chunguzwa.



Jambo lingine mlisema katika Baringo Central ni kwamba, Baringo North, sorry, Baringo North, The Constitution should provide that Clan Elders shall solve land disputes. Kwamba kuna case ndogo za kinyumbani ambazo hamungependa ziende kwa hii koti ya hii makoti yetu ya mawasili ya sheria ngumu. Mungependa kesi ambaye inasikizwa katika mashinani, manyumbani na imalizwe bila kukuwa na hii sheria ngumu ngumu kutoka Uingereza. Kwa hivyo Tumesema hivi: kutakuwa na koti ya aina mingi, Supreme Court, Court of Appeal, High Court, na koti ile ndogo ndogo halafu article number 2185, sub article (3), any tradition or local tribunals with jurisdiction in issues of local significance.

Tuwe na makoti ndogo ndogo ya wapi ya kinyumbani. Na wapewe nguvu kutatua mambo ya nyumbani. Wazee wafane nini? Maanake hata sasa kuna kesi nyigi kotini wazee wangemaliza hapa nyumbani. Kwa wakiti huu tumekubali kwamba hawa wazee wako na maana katika kazi ya sheria wapewe pia nafasi kutatua haya mambo. Kwa mfano sasa kuna sababu gani kwamba mzee akifa at hiyo kesi ipelekwe mpaka kotini, succession ifanywe ipelekwe Kenya gazette Nairobi na kila mtu kwa hii Location wanajua kwamba huyu mzee bibi yake ni huyu mtoto wake ni huyu na huyu; kwisha inaisha. Kwa hivyo ma cases kama hiyo hakuna haja, iende Kabarnet, Nakuru sijui Nairobi Kenya gazette ibaki kwa wazee. Ninaelekea kumaliza.

Hii Katiba ni ya nani, ni ya election hii, ni ya kesho ni ya jana, ama ni ya nini? Tumesema nini Tume, katika page number 2, “We adopt, enact and give to ourselves and to our future generation this Constitution. Hii Katiba ni ya sasa na vizazi vinavyo kuja. Si Katiba ya kura ya 2002, si Katiba ya kura ya 2007, si Katiba ya miaka 10, ni miaka na miaka na miaka. Kwa hivyo tukiangalia tuangalie kwa macho ambayo ni ya sasa na ya siku zingine. Tusiangalie na sura ama kioo ya sasa, kwamba kwangu kwa hii Katiba kuna nini ndani hii itanifaa. Tuangalie Katiba ya mbele, ili tunasema God bless Kenya. Mungu aibariki Kenya. kwa hivyo tunajiweka chini ya Mungu kwa hii Katiba, tunazingizia masilahi ya wale ambao hawako sasa, an pia masilahi yetu sisi wenyewe. Kwa hivyo ni Katiba iko chini ya Mungu ni yetu wenyewe ambako tuko hapa sasa na wale ambao hawako sasa.

In English it is an all time document; ni ya muda ambao hautaisha. Na jee kuna swali kwamba Bunge inaweza vunjwa.

Sisi kama Tume, tuko na mpango gani kuhusu hii Katiba? Mumesikia kwamba kuna watu ambao wameteuliwa kwa niaba yenu, wataketi chini kutoka wiki ijayo kwa mwezi mzima, kila siku kwa siku 30, wakichambua hii document, baada ya maoni yenu leo pia, waichambue waiangalie na waipitishwe. Na hawa watu pia asili mia 30 ya hawa watu ni watu wa Bunge. Bunge ikivunjwa leo ama kesho ama kesho kutwa. Hiyo conference haitakuwa na watu wote maanake hakutakuwa na wa-Bunge.

Kwa hivyo itabidi kwamba hii kazi isimame tufanya kura halafu pengine hatujui. Pengine baadaye Bunge lingine lije na hii kazi tuanze tena kutoka mbio. Imetumia tiyari shilling billion 2, kwa hii kazi. Tumetumia kwa wakati wenyu. Tumetumia rasilimali zenu, maanake kama Committee yenu imechanga pesa yake kutoka hapa kutumia kwa hii. Kwa hivyo kama ni fedha na muda tunge hesabu, ingekuwa billion nyingi zaidi. Na sisi kama Tume ingekuwa ni haibu kwa nchi kama Kenya. Hatuna fedha za kuwalipa waalimu maanake hizo fedha zimetumiwa kwa njia zingine, halafu tutumie billion 2, halafu baada hiyo kazi karibu kwisha iende namna gani, imwagiliwe ile mtaro kama sewage ipotee. Hatuna pesa katika inchi kama hii kutumia vibaya bila kuwa na result.



Kwa hivyo sisi kama Tume tuliomba kwamba na Tume omba kwa mtukufu Rais mwenyewe, tumeomba kwa Bunge kwamba tafadhali, tungeomba hii kazi imalizwe kabla ya kura inayo kuja. Na mjue kwamba hata kama kura ikipigiwa mwezi wa tatu mwaka ujao haitakuwa si halali, itakuwa halali? Maanake mnajua kwamba Bunge la sasa iliapishwa mwezi gani, mwezi wa pili 1998, kwa hivyo miaka yao tano inaisha lini mwezi wa pili mwaka ujao. Kwa hivyo 2003, tukikaa mpaka mwezi wa pili Bunge itakuwa na miaka yake ngapi---- na umewapatia kura miaka ngapi? Hapana miaka nne na miezi sita, mwaka ngapi? Kwa hivyo kama ingewezekena kweli wa-Bunge wamalize kazi yao, hii sheria ipitishwe halafu Bunge ivunjwe nas tufanye elections under hii Katiba mpya. Na pia sisi kama Tume hatutafurahi kwamba kazi yetu kazi yenu haitakuwa ni kazi bure.

Jambo la mwisho kabla sijafungua kikao kwa maoni, ningependa kuwashukuru sana kwa maoni yenu mara ya kwanza tulipokuwa hapa, kwa kuja hapa leo, kwa kutusikiza, maanake hii Katiba inaitwa: "The People's Choice"- uamuzi wenu wenyewe. Kama ingekuwa uamuzi wa Tume sisi tungeketi Nairobi na magari kubwa kubwa kama haya, na ma suit safi safi na ofisi ambao iko na air conditioning chai, ya masala, na mahamri ya kutoka Mombasa na kuandika Katiba katika Board Room.

Lakini maanake si yetu yenyewe, maanake ni watu wa Kenya, ndiyo Tumekuja chini ya mti, mbele ya jua, zaidi ya Kabartonjo maji ya Kabartonjo, mtuambie kuna makosa gani kwa hii Katiba, ama hamna makosa katika hii Katiba, maanake ni ya nani? Ni yenu, si yetu hii. kwa ikipotea itakuwa ni kazi yenu inapotea, kwa sababu sisi nai watumishi wenu kama waKenya. Kazi ya kuandika Katiba kwa wanasheria ni rahisi sana maanake tungeketi chini kwa ofisi fulani watu 15 kwa wiki mbili, na tukachora Katiba, lakini hata hiyo Kenya, hajjakuwa kitu mnaopenda nyinyi wenyewe, lakini sasa, mumedumika kusema ni Katiba yenu nyinyi wenyewe. Kwa hivyo nimewashukuru. Na kwa niaba ya wenzangu ambao wako katika vikao kama hiki ni nchi nzima Kenya leo, nimesema nimeshukuru sana. Na kwa vile pengine baada ya sasa hakuna nafasi ya kurudi tena katika area hii, nimesema asante wacha nisema kama mimi mwenyewe, na kwa niaba ya mwenyekiti ya Tume na wenzangu, tumewashukuru sana na pia asanteni sana kuja na kwa kunisikiza, Mungu azidi kuwabariki, asanteni.

**Elijah Loiero:** Asante sana Commissioner Isaac Lenaola, asante sana kwa kutueleza, kwa kutupitisha katika Draft Constitution, nafikiri kwa juu, juu tumeyaelewa yale sehemu muhimu ambayo wenye bado kusikia katika hio Draft Constitution. Sasa nafasi hii ninapea wananchi, mtoe maoni yenu pengine ni swali ama kuchangia, sasa nafasi hii ni yenu, ili Commissioner anaweza kutupea maoni yake ama majibu yake, kulingana na hiyo swali ambao ulikuwa ume uliza. Kwa hivyo nafasi ni wale watu ambao wana maswali, kama mtindo wetu kawaida, tutachagua watu wanne, watano halafu watakuja hapa karibu kwa sababu ya recording halafu waulize yoyote maswali wako nayo, wako nayo ama wachangie. Mtu ana contribution ama waseme swali mbili. So huyo ni wa kwanza, ninafikiri tuanze upande moja halafu tuende hivi.

**Elijah Loiero:** Na uharakishe kidogo kwa sababu muda ninaona saa ----

**Gideon Limo:** Jina langu ni Gideon Limo. Niko na swali. Swali yenyewe kuhusu vile umesema election of DC. Huyu D.C akichaguliwa na sote tunaolewa kuwa mahali kama hapa Baringo sasa tuko na ma-ka-committees kwa mfano TuRaise, hawa Turaise ni wachache, na kwa mfano nyingine tena kama Watugen. Watugen tuko wengi. Sasa tutachagua aje huyo DC ili atumikie hata wale wa Tuaise. Labda pengine jamii nyingine kama wako wengi. Wanaweza kuchagua huyo DC kwa manufaa yao wenyewe. Sasa ni hivyo wafanye aje ili hata wale wafaidike kwa huyo DC?

**Com. Lenaola:** Sema jina.

**Kennedy Kiptala:** Kwa jina mimi ninaitwa Kennedy Kiptala. Sasa mimi maswali yangu ni kwa upande wa Chief na hiyo ya DC, halafu elimu na uchaguzi wa Parliamentarians. Sasa, wacha ni anzie kwa elimu, education. Sasa tumesema katika hii Katiba mpya, elima itakuwa ni ya bure na ni ya lazima. Sasa mimi mwenyewe nilikuwa ninaonelea, kama tukifanya ikuwe ni ya bure nani lazima, itamaanisha, tutahitaji fedha ambayo itagarimu hawa watu wote, kwa vile hata sasa kwa Kenya, waalimu wamegoma na hatuwezi. So, inamaanisha hii Katiba tuikitengeneza na tuweze kuimplement iende kwa accounts floor hakuna kitu tutakuwa tunafanya. Ya pili ni kwa upande wa Chiefs na DC. Vile mwenzangu amesema, tunataka DC atoke kwa serikali, na serikali iwe inatowa DC, halafu Chiefs iwe ni wananchi wanachagua. The same point, kwa vile tukichagua DC, ita-favour wale watu wana chagua, wengi wenye watakuwa wanachagua ndiyo itawasaidia. Lakini wenye hao, tusema kama hiyo communities minor haitawasaidia, kwa sababu every time waki raise some points, wale wengine wanakuwa ni wengi.

Haya, kwa Parliamentary, mtu akisema Mbunge akichaguliwa, na aende Bunge, halafu aende akae pale, asije atumikie wananchi. Sasa ile percentage imetolewa kwa hii Katiba mpya kusema maybe 30 percent waseme huyo Parliamentarian arudi, a revokiwa, akuje nyuma na watu wakatae. Sasa mimi nilikuwa nataka hiyo percentage irudishiwe. Kwa sababu let us say, 30 percent ya North Baringo voters ni kitu kama fifteen thousand ama 16 thousand. Sasa hawa watu kupatikana halafu wa-report kule Bunge ni ngumu. Inataka irudi chini ikuwe kitu kama ten thousand. Halafu ya mwisho----- no ikuwe kitu kama 10 percent ama 15 percent.

**Elijah Loiero.** Sema jina

**Alfred Komen:** Asante sana. Kwa majina ni Alfred Komen; asanteni Commissioners kama vile mumeingia na wakati tulikuwa hapa vile mlisema, ni yale ambae tuliwahi ku contribute wakati ule, na wakati huu sasa mume turudia tuone ya kwamba tuzidi kuyachangie tena kabla hii sheria iende. Sasa kwa upande wangu, yale ambaye ningetaka kusema ni kwamba kwa Provincial Administration tunaona kwamba wale ambao kutoka Location Village, inaenda kwa Location, inaenda kwa District mpaka Provincial, mpaka National walikuwa wakisaidiana na Provincial Administration.

Wale wa village, wa Location, wa District, wakishindwa, kama Village Elders, kuna administration ambaye ni official. Sasa ikiwa mambo yote yanaenda kwa election, ninaona kama kutakuwako na hitilafu fulani, kwamba kama sasa hakuna mtu ambaye ni independent, kama Chief, wakati alikuwa kwa upande hiyo. Sasa ikiwa ni election, mtu atakuwa aki bembeleza wale ambao walimpigia kura, kwa sababu itakuwa ni ya kupitia kwa kupiga kura, ndiyo sasa ulinzi wa haki wa wananchi itazidika, kwa sababu itaenda kwa njia ya uchaguzi. Haitakuwa na utafauti yoyote na siasa ya kawaida kama ile ya Council, ya Parliament, and so on. Kwa hivyo ingekuwa afadhali, hiyo Provincial Administration should not be appointed.

Second, hii mambo ya ku-chose President, Ministers, wale ambao si wakilishi wa wananchi, sioni ukweli wa hapo, kwa sababu kila wakati mtu akichaguliwa kutoka sehemu yake, akienda Bunge, sasa sisi, tukiwa kama hapa Kabartonjo, tukiwa na Minister, tunajua anatuakilisha kutoka hapa mpaka juu. Lakini hiyo Ministries kama ni ya appointment, na tunajua appointments zinalingana na level ya education ya watu. Sehemu zetu zingine bado iko chini kielimu. Si kusema ni hapa pekeyake, katika Kenya mzima, kuna sehemu zingine ambao si sawa kielimu na wengine. Kwa hivyo pengine appointments ya Ministers zitaenda kwa wale ambao wame elimika na wale ambao bado hawajakuwa na elimu ya kutosha watawachwa nyuma. Kwa hivyo ingekuwa bora system ya kwanza ambaye tunachukua kwa kutoka kwa watu wetu ambao wanatuakilisha ili distribution ya Ministers isiende katika sehemu mbali mbali katika nchi.

And then kuna moja, Right of Life. Hiyo Right of Life, ikiwa sasa zamani kuna kwa ile Katiba ya kwanza, tunasema mtu akifanya makosa, ikiwa mtu ame uwa mtu, sasa ikiwa sasa inasemwa ya kwamba hakuna any penalty ya tuseme kuwa mtu yule ambaye ame--- au mtu yule ame murder huyo, sasa kuna murder case, ambaye mtu akifanya makosa ya kumuua mwingine, anauwawa hata yeye mwenyewe akipatikana na makosa. Sasa ikisemekana kwamba hakuna jambo kama hilo, si watu watakuwa hawata kuwa na---hakuna kitu ambacho kitakuja kuzuua wasiuwe wengine. Kwa hivyo tafadhali, proposal ingekuwa bora tukisema tunaondoa hiyo, tuwe na alternative. Kwa sababu hatujaambiwa alternative. Kwa hivyo, ingekuwa alternative ndiyo tuwe tukilinganisha ile ya zamani na ile alternative, kwa sababu hakuna.

Sasa kwa Constitution completion, mimi ningeonelea kwamba haingekuwa bora ku harakishwa jambo hili, kwa sababu Constitution itabaki katika nchi kwa miaka mengi. Kwa hivyo ikiwa sasa ita hairishwa kwa sababu ya election, hatutakuwa na Constitution ile ambaye itadumu kwa muda mrefu. Kwa hivyo ni heri hata kama election ikija kesho, Constitution iendelee kwa next Parliament. Thank you very much.

**Elijah Loiero:** Kariabia Mzee.

**Edward Toroitich:** Kwa majina ni Edward Toroitich. Yangu ya kwanza ni kuunga mkono Katiba, Draft hii ya Katiba ambayo inaendelea wakati huu, kwa sababu kuona kwangu, ime husika sana na watu wote, na inagusia kila kabila, kila jamii, na watu wote, wakubwa kwa wadogo kama vile imedhiirisha katika kuandikwa kwake, kwa hivyo mimi ninaunga mkono, ni nzuri na ninasema asante kwa serikal kwa kubali Katiba iandike, kulingana na mapato ya wananchi, kuelekea miaka hizi na miaka zinazo

needle mbele. Kwa maana ile ya hapo hawali, haikuhusika sana na wakati huo, ulitokea we call them in English loopholes. Kulikuwako na mambo mengi, yale wananchi hawakuhusika na wengi wame baatika. Kwa hivyo ninauunga mkono.

Halafu ya pili, ningependa kujua kidogo kuhusu House of the Representatives and hio inaitwa Village Council, District Council, Provincial Council, sijui wajibu wao kazi zao itakuwa namna gani, ita endelea namna gani? Yaani, watafanya kazi na kuhusiana namna gani?. Mengine yalikuwa yameulizwa, ni asante.

**Job Singenye:** Kwa majina ni Job Singenye. Yangu ni kuunga mikono yale imeprofesiwa na kuandikwa na hizi mavitabu ambaye tukonaye hapa. Ingawa hatujasoma na kumaliza, mimi ninaona yale tulisema hapa sijui kama yaliandikwa yote. Kwa sababu hiyo mambo ya Village Elders ama kuletee madaraka ama kupewa wazee wa mitaa madaraka ya kuangalia makesi ya mashamba na kuangalia mambo mengine, mimi ninaona tulichangia hapa. Kwa sababu kuna wazee wanafanya kazi katika village na Chief anakula mishahara, sio hawa, na hawa hawapati kitu. Unaona Chief ana meta meta ana nyeta, akienda kwa DC anaongezewa madaraka mpaka anakuwa Senior Chief, yule anayefanya kazi hiyo ni mzee kama huyu Harun. Na yeye hapati chochote. Hiyo sio sawasawa. Itakuwa kazi gani lakini ninajua wamepewa madaraka.

Jambo lingine niliona hii mambo ya kutoka hapa mpaka Provincial ama District Council, mimi ninaona kuna pahali moja ilichelewa. Tulisema katika Provincial tuwe, na Regional Government, ambaye tutakuwa na Regional Governors, Regional Secretary, Regional Assembly, ambaye tutakuwa na wajumbe pale, hatuna haja ku sema wao watatoka Loitokitok, ama Katigani, ama sijui wapi, ndiyo ---ndugu yangu hiyo sio hoja. Na hio tukasema itakuwa ni bora hawa watakuwa na nguvu, au watakuwa na uwezo wa kusimamia Provinces, au yale mambo yako ndani ya Province hio. Na hawa ni watu watachaguliwa kutoka kila District. Na ingawa tunasema inawezekana. Lakini kama inawezekana, tungependa kama ni wasifiche watu ungene katika Province. Tuwe wajumbe wa zamani. Kwa sababu zamani wajumbe walikuwa ni wachache. Kama darasa inakuwa kubwa inaongezewa.

**Elijah Loiero:** ..... nini.

**Job Singenye:** Bado ninandelea. Inginge ni ya kwamba niliposoma hii kitu juzi, sijui kama ni kuone sikuona vizuri, kuna mahali pengine inasemekana title deed, jina la watu wawili inatakiwa kuandikwa. Jina la baba, jina la mama. Kama huyu sasa ni mamsap wangu, title deed itakuwa kwa jina langu na jina lake. Hiyo niliona sijui kama inawezekana. Mimi nilisoma pahali fulani. Mimi ninasema, unajua nikiona kitu ninasema. Hio maoni isiingie na isitokee kitu kama hicho. Unajua nyinyi mliongea hapa na kuna mahali pengi mlionea. Jambo lingine ambaye mimi ningetaka tena kuchangia na ama kusema ni ya kwamba, nilipokuwa hapa, kuna kitu kingine tulichangia. Tuliona hii mambo ya uongozi, na nikaona tena imeandikwa mahali fulani. Tukaone hakuna haja wale vijana vile vijana wangu walisoma wakamaliza form four, na mimi sikufika hapo, nasema nataka Council yule anataka kugombea kiti cha Council, awe ni mtu ametimu katika form four. Na tukaona vile vile, mwenye uwezo, yule mwenye uwezo, kama kati ya hawa ma-councillors ya hali ya juu, lakini kesho mtoto wake anarudi anasema mimi niko

certificate ya form four, mimi ninataka council, na yeye hawezi pale mbele.

Tukaona hio, juzi niliona language ya Bunge, iko English, iko Kiswahili, na ikasemekana tena ni language ya Taifa la Kenya ni Kiswahili ndiyo imekubaliwa iwe ni National language. Nimeonelea, na ni maoni yangu ya kwamba iwe ni Kiswahili itumike katika Council. Ili tupate watu wa maana, tusiwe hata mkora yule alisomea town anarudi anasema huyu baba yangu amekwisha kuwa mzee mimi ninataka kuwa Councillor. Kuingia huku na huku, anapewa, kuingia huku hata ukimwambia peleka huyo mtoto kwenda kwa kazi mahali fulani, anapitisha njia ya Eldoret, badala kumpeleka Nairobi.

**Elijah Loiero:** Sema ingine.

**Job Singenye:** Ndiyo wenzangu mimi ninapinga hiyo na mimi ninapendeza lugha ya Kiswahili.

Mimi ninaombea hawa watu wa Commission; sina mambo mengi lakini tukona watu wachache hapo hatukubaliwa sisi tuseme maana tulikuwa wazee tunaweza kukosa kuchangia na mimi nikona mbili tatu.

Ingingine ni ya kwamba hiyo mambo ya kusema kama mtu anachelewa kwa Bunge kwa siku hii na siku hii, mimi ninona itakuwa ni fitina. Kwa sababu mimi huenda ikawa sitaki Mbuge fulani. Mimi ninachochea, ninauza shamba langu na kuchochea na watu wananunua, na ninajua ile quorum inatakikana. Huyo anaondolewa ovyo ovyo, na alikuwa ni mtu wa maana, ama ange rekebisha hata life yake. Hiyo ndiyo mimi ninaona sipendi kitu kama hiyo, hiyo. Hiyo itaangamiza viongozi ya haki katika nchi hii. Ingawa tu watu wengine wanapenda hiyo, mimi leo nikiambiwa, vile Councillor amechukua nafasi yako, ndiyo hiyo seria inatumika, mimi ninaweza kufanya madhara, ninaweza kuiba hata pesa kesho na kuondoa yeye. Hayo ni yangu, sina mengi, asante sana.

**Elijah Loiero:** Asante Sana. Commissioner nitapatia huku ujibu.

**Com. Lenaola:** Asante sana kwa haya maswali. Swali la Bwana Limo. Limo anasema kwamba katika wilaya, kuna makabila ndogo ndogo. Na anasema kwamba angependa kuona kwamba kwa hii Draft, kuna njia ya kuangalia makabila ndogo ndogo. Ningependa tu kwa juu juu, kumwambia Limo kama kuna kalamu na karatasi, angalia hizi articles na asome baadaye halafu nitamwambia moja ambaye itamfurahisha. Article number 14, sub article 3, sub article 11, sub article 14, sub article 15, sub article 18. Article 14 yote kuna mambo ya minority zina jaa. Article 77, mambo ya minority. Article 235 (2b) minorities, na article 239. lakini kwa Councils, maanake swali yake ilikuwa juu ya ma-Councils, tunasema hivi. Article number 230 sub article 3 (n) inasema hivi. Sheria ya hizi District, may require government to have rules and mechanisms for the protection of minorities and the promotion of their rights and interest.

Kila serikali katika Wilaya, iwe na sheria ya vile itaangalia maslahi ya vikundi vya makabila ndogo ndogo katika Districts. Kwa mfano, Njuruin katika Wilaya hii, hata ukifanya nini wafanye nini, hakuna siku watapata Mjumbe ambaye atakuwa ni mjumbe

wa njoroi. Maanake kura yao ni kidogo sana. Lakini ni watu wa hapa. na wako na haki pia kuwa hapa. Kwa hivyo tunasema kwamba pia wao wapewe nafasi katika wilaya wasengeti kiwango fulani ya viti katika Wilaya kuangalia masilahi yao. kwa hivyo tunaangalia hiyo swali kwa kikamilifu hapa.

Mwenzangu Bwana Kiptala, mambo ya education, si mambo ya education pekee yake. Kwa hivyo kuna mambo mengi ambao ingetaka fedha. Education, mambo ya afya, hata mambo ya kulipa mishahara za maofisi pia, ni fedha mingi. Lakini kama Tume tumeketi tukaona kwamba kabla ya National Conference, tupate wataalamu ambao kazi yao ni kuangalia hii Katiba vile inaandikwa na kuona what is the cost, gharama kifedha ya hii Katiba ni nini? Halafu pili, jee! hii garama tunaweza, ama hatuwezi? Tatu, tanaweza kufanya vitu fulani bila garama, na garama vibaki ama namna gani? Kwa hivyo hiyo swali ni swali zuri, na sisi wenyewe tumeambiwa kwamba tuangalie hiyo. Na nimeitwa hivi leo jana usiku kwamba ni ende Nairobi maanake kuna wataalamu wa hii kazi ambao wangependa ku zungumza na sisi, tukona Committee ndogo ya hii kazi, na mimi ni mmoja wao. Na baada hapo sasa, siende tena Chemolingot, ninarudi Nairobi maanake mkutano ni kesho asubuhi, kuangalia hio swali ya Kiptala, gharama hii ya Katiba ni nini? Kwa hivyo hiyo swali nitaangalia nikirudi.

Mambo ya Chief na DC, kuwa appointed, elected, hayo ni maoni nisha ya chukua. Mambo ya kuwa na 15 percent na 10 percent ya watu wa Constituency ndiyo kupiga kura, unajua hatupendi kuwa, kumpata mjumbe iwe ni kazi, maanake alipo chaguliwa na akaeshinda, alipwa jukumu kwenda kufanyia watu kazi. Kwa hivyo, siasa ya kumalizana, hatupendi, haipatiwi nafasi katika Katiba. Kwamba mtu akisikia kwamba ameshindwa kesho asubuhi aanze kutafuta signature kutowa mjumbe ambaye amechaguliwa na watu. kwa hivyo nilisema kwamba tufanye hi system ya kutoa mjumbe ni ngumu, na pia ni rahisi. Ukiwa na moyo sana ya kumtoa huyu mjumbe chukua one third ya kura ya hii constituency. Ita watu one third wa ku-support. Kama huwezi pata, basi huna watu. Maanake one third kama hawako na wewe sasa huuna watu. Kwa hivyo kama hapa ukitaka Mbunge atoke, tafuta watu eluf kumi, kama huwapati basi huuna watu, na ukae nyumbani ukunywe maziwa ya ngombe yako. Kwa hivyo tulijaribu kufanya ngumu na pia rahisi.

Mwenzangu Bwana Komen, maoni kwamba to-retain ile system ya sasa ya administration, Tumeichukua kama maoni kutoka si wewe peke yako. Tumezunguka kutoka wiki iliopita kutoka Nanyuki, Samburu, huko Wamba, Maralal, Nyahururu, Kabarnet jana, ile swali la administration kwamba isitolewe inazidi kuja. Kwa hivyo tutaichukua mbele. Lakini nimewambia ukweli kwamba watu wa Kenya, 85 percent walisema nini, waondolewe. Na sisi kazi yetu ilikuwa ku sikiza maoni ya nani? Ya watu wa Kenya. Lakini pia nisema kwamba ni jambo ambalo tutaliangalia tena. Vile ninarudia Nairobi, ninabeba haya mambo kwamba, pengine tuliangalie hilo swali tena kindani, kama kuna sababu ya kutoa, ama kuliacha. Mambo ya Cabinet kuwa Members of Parliament, pia hio tutachukua. Hata wajumbe wenyewe kutoka Nairobi wamesema kwamba wangependa kwamba Cabinet ikuwe kuko Parliament.. Na unajua hivi sasa hakuna Mbunge ambao anaenda Bungeni ana--- bendera, kwa hivyo ukitoa bendera sasa kabla hawajafika hawatakubali. Kwa hivyo hilo swali sasa tutapeleka mbele tuone kama watu wanapendelea.

Mambo ya death penalty. Unajua k`atika Katiba, hatuwezi ku andika kwamba death penalty be remove and be replaced with life sentence. Hiyo ingine ni katika sheria. Lakini kwa proposal yetu hapa tunasema kwamba death sentence itolewe ikiwe kifungo cha maisha. Kwa sababu dini wengi wenu ni wa Kristo. The Bible says do not kill, usi uwe. Na ikisema kwamba ukiuwa pia wewe uuliwe, maanake huwezi kupewa maisha marambili. So tunasema kwamba mtu akiuwa, ama aki nyanganya na robbery iolence, akiwa ndani maisha, aende akule ugali na maharagwe huko ndani.

Mambo ya Bunge, tusema Bwama Komen anasema kwamba Katiba isimame tungoje Bunge likuje, halafu hio Bunge ipitishie hii Katiba. Kuna hakikisho gani kuwa ilo Bunge itakuwa na interest ya hii Katiba, kuna hakikisho? Hamna. Na jana niliwapatia watu wa kaburet mfano mzuri kwa hiyo kazi. Huko Zambia, President Frederick Chiluba, mnakumbuka kale kamutu kafupi, huko wa Zambai, alipotoa kaunda alisema kwamba in my government, I will ensure mukona kaatiba mpya, kwa miaka mitano. Kwa fikirie kutakuwa na Katiba mpya. Alikuwa mtu wa-opposition. Akapewa kura, akaingia kama President. Unajua hii kiti ni tamu saa zingine.

Kwa hivyo alipokuwa na hii Katiba ya zamani ya Zambia, akaona ni tamu sana, miaka akazungusha Commission kama yetu, aka zungushwa, aka zungushwa, after five years hakuna Katiba. Akasema, kulikuwa na siasa kali ya transition kwa hivyo, ningependa mnipatie miaka ingine ngapi, ndiyo niweze kumaliza hii kazi ya Katiba. Baada yamiaka tano, in the old Constitution, si bado ako na ile ya zamani, Professor Ghai aka uliza, huyu Professor Ghai, akaenda huko Zambia, aka muliza President tulikisema kwamba wewe ni mtu wa new Constitution, new beginnings, what happened? Akasema hivi, wakati huo nilikuwa opposition. Sasa niko wapi? Serikali. Na serikali ya sasa haina haja na Katiba mpya. Kwa hivyo hatuna hakikisho kwamba serikali inayo kuja iko na haja na nini, na Katiba. Kwa hivyo ni vizuri Kenya kwamba tushike kila mtu mguu. Wapitishie hii Katiba, lakini implementation ya Katiba, ikuwe serikali gani inayo kuja.

Ndugu yangu Bwana Edward Toritich, ukiangalia article number 230, iko na kazi shughuli za District Council, na nyuma ya hii document katika page number 45, tumepatiana shughuli za District Council. Mambo ya education, mambo ya medical, mambo ya maji, mambo ya barabara, mambo ya planning, agriculture, land survey, licensing, labour, zote ziko katika number 45. Yaani serikali mambo inafanyika kwa Province, tumeleta katika Districts. Halafu Village na Location Councils ni sub-unit za Districts. Kwa hivyo ni kama vile ziko sasa lakini nguvu ziko katika Districts, si katika Province tena ama Nairobi, ziko katika Districts. So all the services za watu ziko katika Districts.

Mzee wangu Bwana Segenge rafiki wangu, mambo wa wazee nafikiri nilisema kwamba tumewapa wazee wa vijiji mahali poa hapa. Lakini zungumza juu ya hio, sita rudia. Mambo ya mashamba mambo ya uridhi wa mali, naye ni katika hali wa wazee, na watalipwa maanake ni sasa ni ofisi ya ki Katiba, si ofisi ile mnafuata fuata Chief kwa shillingi kumi shillingi ishirini. Sasa mambo yao yamewekwa hapo kama ofisi ya Katiba. Kama ni ofisi, basi watalipwa. Hebu wazee kama hawa sasa wamekubaliwa ki sheria. Hapana mambo kufuata watu wa chang'aaa na kuwambia lete ishirini bob, tumekataa.



Mambo ya Federal Government, unajua watu wanasema ya kwamba hii Katiba si ya Majimbo. Hakuna Katiba ki-majimbo kama hii. Jana huyu Mzee Hezekiel wa Msambweni nilimueleza, maana ya Majimbo ni nini? Maana ya Majimbo ni mbili tu, kwamba serikali ije karibu na sisi. Ikuwe serikali ya sisi tuna-control serikali. Pili mali yetu ibaki wapi, kwetu. Na hii Katiba inasema nini? Mali ya Wilaya ni ya Wilaya gani? uongozi ya Wilaya hio ni ya nani?

**Chorus:** Wilaya

**Com: Lenaola:** Iko Majimbo kuliko hiyo? Halafu mzee wangu Segenge ananiambia angetaka kuwe na serikali katika region. Region kwa sasa ni nini? Si ni Province? Haya article 219 inasema hivi, “Legislative Authority of the Province is vested in the Provincial Council. Nguvu za kutoka sheria za Province, iwe katika Provincial Council. Halafu ananiambia, hamna governor katika hii Katiba, Governor wa Province. Article 219 (4). The Provincial Administrator is the Executive Authority of the Province.” Huyu si ni governor? Mnataka mwingine tena kutoka wapi? Hala! Hii ni Majimbo tupu. Haya kwa hivyo Bwana Segenge iko. Isiongoje Majimbo ingine, imejaa.

Mambo ya title deeds, kwa hii Katiba, hakuna mahali tumesema kwamba title deeds iwe kwa joint names za baba na mama. Hiyo ni siasa ambao mimi sijasikia, hiyo ni fitina, ndani ya hii Katiba sijaona mimi. Mambo ya elimu ya watu wa Council, kwa hii Katiba, hatukusema sisi kwamba Location Councillors, District Councillors wakuwe O’level, maanake, ijapokuwa maoni ya watu wengi ilikuwa kwamba ma-councillors wakuwe form 4, tukaona sisi kwamba, katika ma District, katika ma-locations, kuna watu ambao hawana masomo, lakini uongozi wao unatosha katika hio area. Pili masomo Kenya si sawa. Kuna Wilaya ambazo watu wamesoma chungu nzima, kuna Wilaya zingine ambazo, kutafuta mtu wa form four, ni kutowa mtu kutoka akuwe mwalimu akuwe Councillor, na je nani atafundisha watoto wetu? Ama kijana wetu moja ako Polisi ama Jeshi, tumtoe akuwe Councillor, na nafasi ya majeshi hata kuwa huko. Kwa hivyo tukasema hivi. Tuangalie hayo mambo maanake tukitaka form four, kuna mahali tutakuwa na shida ambazo hatuwezi kutatua vile inaweza kuja, kwa hivyo katukusema kwamba Councillors wawe na elimu yoyote, tumewacha open,

Lakini mambo ya lugha, tumesema hivi, article number nine, “The official languages of Kenya are Kiswahili and English, and all official documents shall be made available in both languages. Lugha za ki Taifa ndio Kiswahili na Kiingereza. Na kila documents katika Kenya, iwe kwa lugha ngapi, mbili, na sisi tumeanza kama Tume, hii Katiba yetu itatoka kwa Kiswahili na Kiingereza. Hi report ambao tunaiona hapa sasa yaani Kiswahili yake imetoka. Kwa hivyo lugha ngapi? Kama huelewi hiyo lugha mbili, usingie Council, kaa nyumbani.

Mambo ya kuita MPs, kabla ame miaka mitano lakini nilisema hivi, tulifanya ngumu, lakini pia rahisi. Yule mtu mkora hataikani kwende mbele kufanya kazi, lakini siasa isiingie kutowa mtu ambae ni bure. Kwa hivyo tuangalie nini, both sides. Mtu ule mbaya, tusimuachilie bwana. Maanake tukimwachilia itakuwa pia lawama kwetu. Lakini pia wale mikora ambao wameshinda kwa kura hata kuchukua kiti ya Mbunge, wasipewe nafasi hii straight forward, wapatiwa pia vikwazo. Haya swali zingine tano.



**Elija Loiero:** Okay, tutapea nafasi hii upande huu sasa. Barmosho, Langolati, na mtu yeyote, mmoja huyu hapo, na ule mzee ako nyuma, nafikiri muje maramoja. Mambo ya kwanza, tunahitaji jina, jina lako, halafu ukimaliza kuongea unaandikisha jina kwenye register. Pia wale ambao wameingia, tafadhali muandike jina kwa yuule karani ako pale mahali pa kuingilia.

**Com. Lenaola:** Nina sema hivi, ngojeni kwanza sisi watano halafu wengine watano, kwa hivyo tusikae wote hapo, wale wasichana wa kwanza, wabaki, wale wengine tena wa mwisho warudi pale.

**Elijah:** Ninafikiri tuelewane, kuna wale ambao nime waa-appoint.

**Isaac Chemobo:** Basi jina langu ni Councillor Isaac Chemobo, ninatoka Usen Location. Yangu, vile nimeenda through hii Katiba, ninaunga mikono Katiba hii. Ijapokuwa upande wa Administration tu ambao sikuunga mikono, na watu wengi kwa Location hawauungi mikono Chief aondolewe. Kwa hivyo mimi ninaunga miokono kikamilifu Katiba hii vile inaandikwa, na ningependa kutaja mambo machache tu ya kwamba Katiba hii iendelee ikamilishwe kabla ya elections, kwa sababu election ikifanywa kwa Katiba hii, Kenya yetu itakaa vizuri.

Hasa laini ile ya President, Vice, Prime Minister, and two Deputies, wale wana nga'ng'ania viti hizo ikienda kila sehemu, serikali yetu kwa Kenya ambaye itakuja, itakuwa very stable. Kwa hivyo mimi ningependa tuunge mikono kikamilifu na ku request His Excellency the President asi-dissolve Parliament kabla ya Katiba mpya. Kwa sababu, wale watabaki kabla ya kuenda ni sisi, na kama ni sisi, tunataka serikali ile inakuja iwe stable. Na haiwezi kuwa stable kama hakuna Katiba mpya.

President mpya akikuja kabla Katiba mpya, havezi kusign hii Katiba. Tuelewe kikamilifu, kwa sababu, President yule atakuja, atasema powers, au mamlaka yangu ime shushwa. Kwa hivyo tunaomba His Excellency, akubali akae Parliament isongezwe kama mwezi tatu au mwaka moja, bora Katiba imalizwe. Hii ni manufaa ya watu wa Kenya kwa jumla. Na ninge penda tena kuunga mikono kwamba,, wale Wajumbe tutachagua wawe Ministers kwa sababu kule America wana-appoint ministers kutoka wale si Wajumbe. Lakini sisi tunafurahia wajumbe wetu tukichagua wapewe kuwa Ministers. Ili hata sisi tukiona bendera ikizunguka kwa gari yake, tunajivuna.

Ya mwisho, wale ambao wataenda kikao kule Nairobi kwa siku thelathini, wachunguze sawasawa na wasigeushe mambo mengi, ili ya manufaa ya watu wa Kenya waone kikamilifu, na wasiione kwamba ni watu wadogo. Sisi kama District ya Baringo Tumechagua watu watatu, na tunaimani kwa hawa kwamba wata-represent sisi kikamilifu. Asanteni.

**Elijah:** Asante sana Councillor; next?

**David Boit:** Kwa jina ninaitwa David Boit, kutoka Saimo Location, Kapsigi

Sub-Location. Ya kwanza ninge penda nitowe shukrani kwa watu wa Katiba, kwa sababu wamekuja hapa mara ya pili, ni maajabu, nisikie kamili. Huyu officer ameongea na vile amesema, amesema kamili. Yale maneno tuliyasema juzi na amekuja kusomea sisi a hundred percent, na sijui jina lako unaitwa nani, ehh. Na ni kweli. Ningependa niseme ya kwanza katika Kabartonjo Division kuna mambo maajabu kuhusu mashamba, wale wanapata mashamba, na wale wako na mashamba.

Sasa ninge penda nisema hivi, kama mambo ya kupeana mashamba inapeana kwa Assistant Chief, ama Chief's office ama kwa Wazee wa Mitaa. Tafadhali, mugawishe hapo halafu tujue kamili nani iko na taabu ya mashamba, kuliko kupeana mtu iko na acre 10, anapewa acre 20 tena. Hii ni tabu gani? Na kuna mwingine hana hata acre moja. Ninaona hata Assistant Chiefs wanapeana mashamba. Iko Ngotongoi, wengine wako Kitale, wengine wako wapi?

Sasa wale wame baki, watakula wapi, na wataishi namna gani, na watoto watafundishwa namna gani? Jee sababu mimi nimbefika hapa tufikishe hii kitu mpaka Village Elders, ama ma Assitat Chiefs au ma-Chiefs, sawa.

Ya pili, ni malize tu, ingine imebaki ni mambo ya busaa. Mambo ya busaa haiwezi kwisha katika dunia hii. Lazima itapatiwa laini yake. Hata kunywa namna gani, lazima itoleshe ili watu wakunywe busaa yao kama hauwezi kwishwa.

**Elijah:** Sasa ungependekeza namna gani?

**David Boit:** Lazima ikatwe. Mimi wakati nilikuwa kidogo, watu nilikuwa naona watu wanaweka kazi kwa kulipa shillingi kumi ama ngapi. Huyu ni mtu anaandikwa kazi busaa ipatikane, watu wanakunywa live live. Asante sana.

**Nathaniel Barmoisho:** Kwa majina ni Nathaniel Barmoisho. Na yangu ni ku ona yale yameandikwa, kwa sababu tunayaona vile tulisema hapa Kabartonjo, tunaunga mikono. Kitu tu ningetaka niulize ni kuhusu mambo ya---- kwa sababu hatutakuwa na enough office ya ---- ama wananchi hawatapata draft ninge penda kuuliza kwa mambo ya ufupi kuhusu ministers na MPs. Kulingana na vile mlisema kwa Draft, Minister atakuwa Minister na MP awe MP? Ningependa kuuliza kwamba, Minister atakuwa appointed kwa njia gani ili tuelewe pengine tutapinga kitu ile ingekuwa pengine ni mzuri. Pili ni kuhusu mambo ya Village Government, kwa kuwa tutakuwa na serikali ya Village, na hatutaki kupinga kabla kujua utaratibu zake. Pengine itakuwa bora kuliko hata ile yetu tunasemanga Provincial government. Ili tu elezwe, pengine baadaye tutajua kama gani ni bora, Provincial ama Village Government. Yangu tu ni hayo, tupewe maelezo ili pengine tutakuwa tukiunga ama tukatae pengine, kwa sababu pengine mengine yanaweza kuwa mazuri kuliko mengine. Asante.

**Paul Andany:** Mimi ni Paul Andany kutoka Kipngonginy. Kitu yangu kuchanga, mimi ninataka kwa Katiba hii, zamani sisi ni wazee. Tumeweka Katiba, vijana si kula pombe, na hakuna, na sasa hii kijana wetu, watoto wetu hii, iwekwe kwa Katiba leo. Hiyo Katiba inachunga mtoto wetu, nimekataa hiyo pombe. Unaona watuwetu iko hapa sasa bado kukunywa pombe kutoka

kiti cha mama yao. Unaona vijana wetu tumezaa sasa, wanashinda sisi. Kama hii Katiba inakuja iwekee adhabu kali kuweza vijana wetu. Mimi ninaomba Mungu achunge nyinyi watu wa Katiba, halafu Katiba yenu inakwenda mbele.

**Job Chesare:** Kwa majina ni Job Chesare, kwa jina lingine ninaitwa Lengurech. Swali yangu kwa Bwana Commissionoer ya kwanza ni kuhusu mambo ya mashamba, Lands Act. Kwa sababu kulingana na Memorandum ambaye tuliandika ya kwamba kuhusu hii inaandikwa Right Holder Kulingana na ile ulisoma saa hiyo, hatukusikia Right Holder imefika.

**Com. Lenaola:** Right Holder ni nini?

**Job Chesare:** Right Holder ni kulingana na kama ----- . Tuliandika ya siku ile ya kwamba wenye shamba hiyo, lazima serikali apewe haki yake, na kwa hii Draft Constitution, inaonyesha tu inaenda namnahiyo, lakini haikuonyeshwa kwamba na mwenye alitowea hiyo alipewa nini?

Pili Bwana Commissioner, ulisema kwamba, kwa hii Katiba Tumetumia pesa mingi sana, hii Contitution inaenda kwa Yash Pal Ghai team. Sisi tukiwa hapa kwa jamii hawa wanaketi hapa, tulizunguka kwa kila jamii, tunatumia mguu, na nyinyi mnatumia Nissan Patrol, na Kenya hii, tuliuliza kwamba hii kitu inaitwa Corruption, hata cartoon ya hii Draft Constitution, inauliza kabisa hii corruption tumalize. Jee hii corruption, itamalizika namna gani tusipo andika kamili yanayo tendeka kwa miaka zingine zinazo kuja? Sisi kwa ajili yetu yote hatukupata hii Draft Constitution. Kama ingewezekana, ingeandikwa kama ile ya issues and questions ya Yash Pal Ghai ambao tulishambasha kwa jamii yote. Kama mungetangulia kupatia sisi wananchi hawa waelewe, leo watu wange jaa hapa na wanaelewa kitu wanasoma. Ningeomba tu utupatie sisi ndiyo hawa waelewe. Kwa hayo machache, ninasema shukrani. Mungu awabariki.

**Charles Chepcheny:** Jina langu ni Charles Checheny, yangu ni kucontribute kidogo kuhusu appointment of judges. Bwana Commissioner katika ile appointment of judges, ukiangalia vile wako, ni karibu centralized in a given Province. Hapa kwetu Baringo, kwa mfano kutoka Tukuta- Marmar mpaka Torongo, hakuna Judge, na si kwamba people are illiterate here there are very many learned people. So I am saying this, the appointment of judges should be reflected in the entire country. We should have a judge from Garissa or North Eastern; we should have a judge in Rift Valley, Coast, Central, Nyanza, and Western, even in Nairobi. Lakini kwa sasa ukiangalia Kortini kule, almost 75 percent are from Nyanza and Western, which is wrong. Thank you.

**Com. Lenaola:** Asante sana kwa hayo maswali, wacha ni anze na hii ya mwisho manake it is a very impacting point. Mimi ni Wakili, kwa hivyo ninajua sana mambo ya Majaji. Na vile Mzee amesema kwamba 75 percent ni kutoka Nyanza na Western Provinces, that is true. Na kwa hii Katiba, tumesema kwamba, appointment to National and Constitutional Offices lazima iwe na Regional balance, ili kwamba tusiwe na ofisi fulani ambao kutoka chini mpaka juu ni one region. Na hata sasa Wakili wanaingia kila mahali. Hakuna Wilaya haina wakili, hakuna Province haina Mawakili, kwa hivyo I agree with you Mr.

Chepcheng, kwa kuona kwamba ni lazima kila ofisi iwe at least a national outlook in the offices. Tusiwe na watu ambao ni ofisi moja ni watu fulani. So hiyo ilikuwa very important kwa sababu mimi ni mtu wa ofisi hiyo, nime sema hiyo kwanza.

**Elijah:** Halafu kusaidia Commissioner, hata katika Tume wa Marekebisho wa Kenya, walichukuliwa kulingana na regions, kulingana na Provinces, hakuna Province iko na zaidi ya mwenzako.

**Com. Lenaola:** Hasa katika Tume, kila Province iko na Commissioners 4, kila Province. Kwa hivyo hakuna Province, except North Eastern, ambao iko na Commissioners wawili. Lakini zile Provinces zingine 7, tuko 4, mimi nikiwa mmoja kutoka Province hii.

**Isaac Chemobo:** Chiefs, D.Os, D.Cs, P.C. wakuwe retained, ndiyo nimesema kwamba, hiyo maoni iko kila mahali, kwa hivyo nitachukuawa tu kama maoni ambayo mumetupatia. Nitaomba Katiba kabla ya election, I think tutazungmuza hayo. Sectors ya government, Tume tuta clarify. Cabinet nje ya Parliament, hiyo pia ni maoni, na hiyo maoni tutachukua tena. Delegates wale ambao wametumua kuja kwa Conference, mjue kwamba nyinyi ni wakilishi. Kwa hivyo wakija pale, hawatakuja na maoni wenyewe. Wanakuja na maoni ya Wilaya. Na sisi kama Commissioners, kazi yetu ni kuona kwamba hawa hawalalii masikio mbele. Kwa hivyo tutakuwa tunawasukuma na kusukuma na kuwaonyesha njia, manake sisi tumekuwa wapi? huko. Kwa hivyo hawako peke yao. Sisi kama Commissioers wa Rift Valley, kazi yetu ni kufanya nini, haya maoni mnaochukua hapa mimi kwanza ninayashika kwa mikono. Hawa wakisleki, mimi ninasema kwa sheng' mimi ninaweka hawa pressure. Kwa hivyo namshukuru kwamba umesema hio.

**David Boit:** Mambo ya pombe ni mambo ambayo tumekuwa tukizungumza ki sheria. Manake mambo ya ulevi, yako na mambo yake kali Tulisema hivi, hatuwezi kuandika kwenye Katiba kwamba wakunywe pombe ovyo ovyo, lakini tulisema hivi, ile pombe ambao ni ya kimila, ile pombe ya saa moja mpaka saa kumi na moja, hiyo si pombe ya kimila. Ama kuna mila inatowa mpaka watu wakunywe pombe ya kila siku? Tumesema kwamba, kama kuna sherehe mahali fulani, basi wazee, ndiyo ni kusema kwamba kuna sherehe kwa family hii leo.

Sherehe ikiisha pombe ina fanya nini, inaisha. Hapana kunywa pombe leo na kesho, unasherekea nini kilasiku mwaka mzima? Hiyo ni ulevi wa kupindukia. Kwa hivyo, Mzee Paulo, niko furaha kabisa. Pombe ya kila siku, hatutakubali, maanake vijana wanapotea. Kwa hivyo si kusema kwamba Katiba imesema watu walewe, hapana Bwana. Sikusema hivyo mimi. Nilisema kama kuna mila ambae ingependa pombe kwa hiyo sherehe, basi kimila ni wazee ni wana fanya nini? Ndio control hayo mambo. Na ni wazee pekee yao, vijana hawakunywi hiyo pombe. Hawana mahali pale. Kwa hivyo ni kweli ni pombe tuwache. Haya, unajua leo karibu nikuwe muubiri.

Mambo ya arthi, mambo ya land allocation, itafanywa kwa wazee. Na katika article number 235, Tumesema, no, this is

Community land, and this is the same question imeulizwa na Chesaro. No, they are different. Tuseme mambo ya katika family tuwachie wazee katika Location tuwachie wazee.

**Nathaniel:** Mambo ya Cabinet and MPs,. Katika article number hebu niseme kwa kirefu kidogo maanake ni swali ambao nitarudi tena. Nani ana appoint Cabinet? Article number 175. The President shall appoint the members of the Cabinet in accordance with recommendations of the Prime Minister, and with the approval of the majority of the Members of National Assembly. Lower House, National Assembly, Prime Minister, na President ndio watafanya kazi ya Cabinet. Prime Minister ana-recommend kwamba watu fulani ningependa wawe Ministers. Prime Minister anapelekea President. President anaangalia recommendation ya Prime Minister. Together with the Prime Minister, wana kubaliana na list ya Cabinet Ministers. Halafu, wapelekee Bunge. Bunge ikiona kwamba mtu fulani ni mkora, si mtu ambaye anaweza kuwa waziri Bunge inakataa. Inamwambia Prime Minister Rudi tena, tafuta mtu mwingine. That is the structure sisi Tume propose. Ili kwamba tusiwe na mtu ambaye anakuwa minister na hafai kuwa waziri.

Jambo la pili, tunasema kwamba kuwe na wizara kumi na tano pekee yake. Kwa sababu gani? Hivi sasa tukona Cabinet 25, na kuna kusema ukweli, hii Cabinet kuna ministries zingine ambazo hazina maana kuwa Ministry. Kwa mfano, Ministry of Vocational Training. Ni Ministry ya village Polytechnics. Inge kuwa under Ministry of Education. Ndiyo tunasema kwamba kuna ministries ambazo hazina maana. Wacha tuwe na ministries 15 za clear na iko na kazi kabisa. Na pia tuna save pesa za mishahara, na magari kubwa kubwa kama hizi. Maanake kila Minister ana marcedez, PS Patrol, hizo fedha ingetumia kwa ministries zingine kufanya kazi za ministries.

Tatu, Cabinet, tumesema kwa hii Katiba, mtu akuwe Minister kwa Ministry ambayo ako na training ya hiyo Ministry. Maanake sioni sababu mimi kama wakili nifanye Ministry wa agriculture, mimi ninajua nini ya agriculture? Na mimi ni mfugaji wa ngombe, hakuna kahawa Samburu sisi, na hatuna majani chai. Ukiniambia mambo ya beans na farmers ya mahindi, sisi hatuna mahindi sisi. Kwa hivyo waziri akuwe waziri wa area yake. Ama mtu wa Jeshi akuwe Minister of Health, anajuwa nini juu ya health? Na kuna daktari chugu nzima Kenya.

Kwa hivyo kila waziri akuwe professional kwa ministry yake. Kwa hivyo kwa hii Katiba Tumesema kwamba professionals in the profession in their areas, tusiweke watu ambao hawajui kazi ambavyo weanafanya. Mambo ya Village Councils, ya Districts Councils, I think Bwana Barmosho, I will just ask you to sit down na usome pole pole article 219, article 227, article 230, and article zaidi.

Article 230 inasema Legislative Provisions afor devolution. Serikali inafanya nini kwa Wilaya, serikali inafanya nini? Na pia page 45, kumejaa shughuli ya serikali za National na serikali ya chini. Serikali ya National mambo ya Finance, National Finance, International Agreement, Foreign Affairs, National Defence. Lakini services ambazo ni za watu peleke kwa District Council. Kwa hivyo tukiangalia hizo it should be very clear kwamba mambo ya national ikae national. Mambo ya services

zetu, maji, why should water be the reserve of national government, maji iko wapi? Wacha ije wapi... mambo ya nursery schools, mbona ikuwe Ministry of Education huko? National schools zikuje hapa. Mambo yetu za family yetu za karibu, mbona isitoke Nairobi, give us money, we make our own roads here nyumbani.

Mambo ya ma forest, article 234,

- (b) Article three, the following descriptions of land is Community land.
- (c) All land, held managed or used by communities, as forests, water sources, grazing areas or shrine.

Ikiwa forest iko kwenu, hiyo forest iwe land ya hiyo community. Na ni hawa tu wazee wao wa village watamange mambo ya hiyo forest. Ikiwa katika hiyo area yenu, mkona maji fulani. Kama vile chemchem za maji. Kuna njia za kimila za kutumia chemchem isi kauke. Wache hiyo community yenyewe iwe in charge ya hiyo maji.

Kama kuna mahali pa kuabudu, unajua kimila kuna mahali wanawake wanaenda kuabudu chini ya mti fulani, ama mlima fulani, iwe ikuwe chini ya hiyo community. Si kazi ya Ministry of forest kuja kutuambia tuabudu mungu wetu mahali gani. Ama Ministry of Wild Life ituambie tuchunge wanyama wetu namna gani. Na kabla Ministry of Wild Life kuja, tulikuwa na hawa wanyama sisi hapa hapa. Kwa hivyo Tumesema kwamba mambo ya community kuwe zaidi kuliko mambo ya serikali kubwa kuja kutuambaia bila kutumia lasirimali mali zetu.

Mambo ya corruption, hii Katiba iko na provisions tele tele kuhusu corruption, kwa sababu gani? Kenya ni number ngapi kwa dunia?

**Chorus:** Number tatu:

**Com. Lenaola:** Kwa kitu gani? Kwa ufisadi, ni aibu sana. Badala kuwa number three kutoka bottom, ni number three kutoka juu. Kwa hivyo Tumesema nini kwa hii Katiba juu ya hii Corruption? Article 14-sub article 6, page number 5.

The republic shall take effective measures to eradicate all forms of corruption. Ni jikumu la serikali kuona kwamba ufisadi katika nchi unaisha. Lakini si hio tu. Unajuwa kulikuwa na Anti-corruption Commission halafu ikafanyiwa mambo interesting, ikauuliwa. Sisi tumeona kwamba hio Commission irudi sio nje ya Katiba, lakini ndani ya Katiba. Article 289, there is established the Ethics and Integrity Commission. Commission ya Ethic and Integrity. Na kazi yake ni yipi? Sub. Article (f), put in place measures aimed at the prevention of corruption. Commission ambaye kazi yake ni kuona kwamba kuna njia za kukataza mambo ya ufisadi. Pili investigate instances of corruption. Ita investigate ufisadi na kuwa pereka kortini. (g) Educate the public on the dangers of corruption. Tufunze sisi kwamba corruption, mwenye kupeana na mwenye kuchua. Kwa hivyo sisi kama wa Kenya, tusi-carry in rushwa maanake sisi ndiyo tuna propagate hiyo corruption. Na kazi ya hii Commission ni hivyo hivyo.

Nne Tumekuwa na kitu inaitwa, kwa hii Kaatiba, leadership and integrity court, page number 45. Kabla mtu kiwa kiongozi katika Kenya, ni sharti uandike na usign kitu kinaitwa Leadership and Integrity Code of Conduct, na jambo kubwa hapa ni kwamba utasema ni mali yako ulitowa wapi. Ukitaka kuwa kiongozi utatuambia mercedes tatu, lorry kumi, nyumba tano na Account kubwa ngambo ulitowa wapi na mshahara yako ni 40 thousand kila mwezi. Ili kwamba tufungie ufisadi nini, njia. Kwa sababu, na jambo la pili, ukitaka kuwa Deputy Secretary, Permanent Secretary. Minister, Prime Minister ama President, pesa zako zitatoka ngambo ikuje Kenya. Kwa hivyo accounts za ngambo tunazifunga, kwa sababu gani? Accounts za ngambo ndio barabara ya ufisadi. Unakula barabara na hulipwi Kenya, unalipwa wapi? Kwa hivyo hata tukitafuta account yako hapa, hakuna pesa kama hizo. Lakini huko ngambo zinajaa tele, zime jaa. Kwa hivyo hizo utatuambia kama ziko, kama ziko pesa ikuje wapi, wapa. Kwa hivyo tumefunga pia njia za ufisadi, kwa hivyo ndugu yango Chesaro, tumefunga njia ya ufisadi.

Tumeomba msamaha kwamba hatukupata nafasi ya kuzungusha hii Katiba kwa muda mrefu, kwa sababu gani? Kwa sababu, kabla mwezi wa nane, sheria ilikuwa kwamba hii Katiba izungushwe katika kila constituency kwa miezi mingapi? Miezi miwili. Lakini mwezi wa nane, Bunge ika rudisha sheria kwamba hii Katiba izunguzwe katika kila constituency kwa mwezi gani? Kwa hivyo makosa haikuwa ya Tume.

Makosa ni ya Bunge ku-reduce ile muda ya zungusha. Lakini kabla ya 28<sup>th</sup> hivi sasa iko tayari to publish hii document kwa njia kama hii, kwa Kiswahili na Kiingereza, ili kama kuna mtu ako na maoni ya kutowa kabla National Conference, mnatuma direct kule kwa Commission, msembe mkona swali kuhusu hii Katiba. Kwa hivyo Tumesema poleni lakini hatuna muda wa kuizungusha, lakini asante kwa kusema kwamba tumeizungumza, tumejaribu. Sasa kwa vile sauti inapotea, nimezungumza namna hii kila wiki tangu wiki iliopita, nimeingia Commission nikiwa kijana mwenye nyuele nyeusi, imekuwa nyeupe sasa, nina fikirini nitachukua maswali nyingine tano wa mwisho halafu nitafunga nielekee kazi zingine. Moja, mbili, mbili hizo nita chukua na sauti pia nita pelekea bibi kwa sababu sijaona bibi wiki mbili bwana.

**Erick kadale:** Okay kwa majina ninitwa Erick Kadale. Pendekezo langu ni ya kwamba hii uchaguzi wa mwaka huu ifanyike katika Katiba mpya. Secondly, tunaona wa Kenya, siku hizi tunaona tuna poteza wakati mwingi sana kwa mambo ya public holidays. Tunaona ya kwamba by the year tutakuwa na 365 Presidents, tutakuwa na maholidays mingi sana. Kwa hivyo kitu ilioko pendekezo langu ni kwamba tunataka sisi wa-Kenya tunapoteza wakati wetu na pesa mingi kwa ku-celebrate ile public holidays. Tunatumia ile wakati wetu tungetumia kufanya kazi nyumbani ama mahali pengine ama popote unafanya kazi, tunatumia kwa hizi, tuna waste kwa mambo ya public holidays. Kwa hivyo pendekezo langu ni tuwe tu observe international holidays pekeyake. Na hii mambo ya Jamhuri days, and the like, ninifikiri hizo tunapata kwa mashule, siku hizi watoto wetu wanasoma na huku wanajua tumepata uhuru mwaka gani, President ya kwanza ilikuwa mwaka gani, kwa hivyo hio tunajua kwa history. Hiyo ndio ilikuwa pendekezo yangu.

Secondly, ni katika role ya Councillors na ma-Chiefs, mimi sijaona tukiambiwa role ya ma Councillors ni hiki na hiki, na tena



ma-Chiefs. Sisi tukiona kwa mtaani, Chiefs na ma councillors, saa zingine hawaendagi laini moja. Mwingine wanaenda njia ile, ingine huku. Sasa tunataka tujue roles ya ma-councillors na ma-Chiefs in gani? Asante, yangu ni hayo tu.

**Michael Kipkebut:** Jina langu ni Michael Kipkebut. Ninayo statement ingine ya ku-make. Ya kwanza tiyari mwenzangu ametaja kuhusu national holidays kwamba hii tumeona Katiba day. Sisi wale tumeketi chini, tukaona haina haja. Ya pili ni chapter five kwa hiyo Bill of Rights, Cap 7 (g), kuhusu watoto. Tungeona kwamba kweli hawataki watoto wasipewe punishment. Lakini sisi tume recommend there should be limited corporal punishment in primary and lower forms in secondary schools, and we based this one katika kitabu cha Biblia Proverbs 23, verse three, 22 verse six, and 13 verse 34. In Proverbs, we based this one kwamba watoto wapewe adhabu ilio sawa kulingana na bibilia. Hapo tunaenda kwa article 38, tuna kubaliana kabisa, one to five. Lakini tungetaka iignizwe kwamba watu wanapoowana katika Constitution there should not be unnatural marriages where we have homosexuality is legalized and lesbianism. There should not be anything unnatural.

Halafu tunaenda just a side pia article 44 (1). Freedom of Religion, beliefs and opinions. tungetaka isome hivi. "So long as it is respect, and dignity and value to all God given human lives." Halafu tunaenda kwa elimu, article 58 (2), tungetaka I include compulsory and there should be compulsory, because inasema, masomo lazima iwe ya lazima na free kwa primary na secondary. Meaning tungetaka iongezwe free for free primary schools, na waalimu pia waandikwe na Ministry of Education if that is of concerned. Otherwise tunasema we appreciate this Draft Constitution and it is a well done job, this should be used in the next general election. Thank you.

**Com. Lenaola:** Thank you very much. Let me speak about mambo ya national holidays,. Unajua hakuna Jamhuri ambalo haliwezi ku heshimu siku zake za ki taifa, lakini kweli ni kwamba tukianza kumpatia kila mtu siku yake ya kitaifa, tutakosa kazi. Sababu tuhesabia national holidays, Christmas, Labour day, Idd Ul Fiddr, Idr Has, Idr Hack, tukihasabu zote basi tutakuwa nyumbani. Na pia ukiweka ile ya Wahindi diwali, pasaka, tutakaa nyumbani mwaka mzima tukikula holidays. Kwa hivyo tumesema sisi hapa kwamba lete hesabu, kwa sababu nchi ya Kenya pia ikona siku zake za kitaifa, tuwe na siku yetu ya Jamhuri, na siku ya Madaraka. Na si ati tuseme kwamba tuwe na heroes day. Kwa hivyo heroes day, Kenyatta day, Moi day zote zikuwe siku moja fulani katika nchi. Lakini tutayachukua maoni kama hayo pia.

Mambo ya roles na Chief na Councillors. Mjue hivi kwa hii Katiba hakuna Chief. What we have ni Council. Kuna wazee katika Sub-Location wanaita Village Council. Kuna wazee katika Location, ambao wana chaguliwa na Village Council, wanaitwa Locational Council, na mmoja hawo atakuwa Chairman wa Council. Halafu kutoka kila Location, kuna wale wanachaguliwa moja kwa moja kwenda kwa District, wanaitwa District Council. Kwa hivyo hakuna mahali kwa Chief hapa. Kwa hivyo ukiniambia ati kazi za Chief, hakuna chief. Kuna Councillors pekeyao kutoka village mpaka district Mambo ya--lakini nimesikia maombi kwamba, kuna mzee walisema kwamba machief tuwa-retain. Kwa hivyo hayo tuna chukua, lakini nilikuwa nina explain, lakini maombi kama to retain ma Chiefs, pia nitachukua.



Mambo ya Biblia kusema kwamba mtoto apewe kidogo kidogo hivi ninafikiri tumechukuwa. Ninafikiri Bwana Kipkebut has a very important point. Unajua katika Nairobi, siku hizi tunapata watu ambao mama anowa mwengine, kijana anowa mwengine, na hio si mila ya ki Africa, na ni laana katika mila ya ki-Afrika kwa mambo kama haya yafanyike. Kwa hivyo kuniambia kwamba tuandike katika Katiba kwamba tukiwa na hayo marriages ninafikiri it is a very very important point. Tusiwache hii Katiba ikiwa open aimlessly.

Kwa sababu tukisema kwamba parties to a marriage are entitled to equal rights in a marriage, inaweza kuwa pia ni mwanamume na mwanamume, au mwanmke na mwanamke. Kwa hivyo I agree with you totally. Tufunge hiyo loophole na tusema kwamba except--- I agree with Mr. Kipkebut kabisa kwamba tufunge nini, hii laini mtu asitumie kusema kwamba mimi ni party na huyu ni party kwa hivyo tukona in marriage. Tusifanye kwa sababu inaleta madhara katika nchi. I agree with you totally. Nita peleka.

Mambo ya religion addition kwamba tuwe na respect dignity and God given Life, I agree. Article 58 juu ya elimu, in fact katika hii, Bwana Kipkebut, katika hii document mahali nimeona imeandikwa primary, you must follow it up to primary. Kwa hivyo rights za elimu ni pre-primary na primary. Kwa sababu huwezi kuingia primary bila kuingia pre-primary. Hii ni makosa, ni error.

Kwa hivyo mahali iko primary ni pre-primary.

Basi nimefika mwisho wa kikao. Wacha niseme tena kwamba asante kwa maoni yenu, yale mumetueleza, yale mumeuliza, yamechukuliwa na huyu kwa mikono, amechukua huyu kwa kunasa sauti. Yote yataingia katika National Conference, and itakuwa debated na kuongea katika hii Draft. Kwa hivyo tutaangalia ---- ikiwa ya mwisho mtaona yale mumesema hapa pia yatakuweco kama ya zamani. Kwa hivyo nikimaliza, tuzidi kuombeana, mtuombe, tutawaomba, ili kwamba hii kazi ikuwe kazi ambao tunafurahia na milele.

**Elijah Loiere:** Commissioner asante sana. Ninafikiri nikona ombi moja Bwana Commissioner. Ninaomba uelezee wananchi seriousness ya situation ambao tunaelekea kwa upande wa Parliament, maybe they want to hear ninafikiria hawajajua mwelekeo wetu. Please maybe just emphasise

**Com. Lenaola:** Mzee baba wa Taifa amesema kwamba, angependa kwamba avunje Bunge ya ile meeting ya Kasarani. Si Kasarani imeisha? Kwa hivyo tukichukua maneno yake, Bunge inaweza vunjwa wakati wowote. Hata pengine nikikaa hapa imevunjwa. Na ki-sheria katika Katiba ya sasa ni haki ya Rais. Kuvunja Bunge wakati wowote. Sections 9, inasema kwamba the President may dissolve Parliament at any time. Rais wa nchi anaweza kuvunja Bunge wakati wowote. Kwa hivyo akivunja si makosa, maanake ni haki yake ki sheria. Atakuwa anafuata sheria ya Katiba ya sasa. Lakini sisi kama Tume tume propose kwamba, na nimewapa ule mfano wa Cheluba, kwamba tusimpe mtu nafasi ya kufanyia ile Katiba ile mpango wa Cheluba. Hii Bunge la sasa limekubali kwamba ni hawa walianzisha kazi ya Katiba, si hawa ni waliteua sisi? Kwa hivyo ni

jukumu lao kumaliza kazi walianza. Tusipatie kazi watu ambao hatuwajui.

Maanake tukienda elections sasa na tuchague wa-Bunge wengine ambao si wale wa sasa, tunajuaje kwamba watakubali hii Katiba, hatujui. Kwa hivyo tumeomba na tushamuelezea Rais kwamba tungependa aongoje kidogo, tumalize Conference mwezi wa 11, Bunge ipitishie hii Katiba mwezi wa 12, avunje Bunge mwezi wa 12, na election ifanywe mwezi wa ngapi, ---? Itakuwa ya miaka mitano ya Bunge, maanake Bunge inaisha mwezi wa pili. Kwa hivyo itakuwa katikati ya sheria ya sasa na pia hii ikona nafasi yake. Lakini, akivunja Bunge, tutafanya nini? La kufanya ni hili. Tutafunga ofisi ya Tume, tutafunga National Conference, twende manyumbani.

Tarehe tatu mwezi wa kwanza mwaka ujao, sheria inayo unda Tume na hii kazi inasema kwamba hii kazi itakuwa imekwisha ki sheria. Kwa hivyo, tutarudi mahali tulikuwa 1998. Mwaka ujao kwa hivyo tutaongoja tena kama Bunge mpya itakubali itakuwa na sababu ya kuanza hii kazi, itatunga sheria mpya tena na kuunda kiumba Tume lingine mpya pengine mpya, ama sisi tuambiwe turudi kazi, halafu kazi ianzwe na kutoka na square zero, na kazi ikwishe. Au sivyo, kama lile Bunge halipendi kazi kama hii, basi hii kao itasaulika milele na milele. Na hio pesa tumekuwa muda wenu kama sasa itakuwa imepotea. Kwa hivyo tungependa kuomba kwamba hii Constitution ipewe nafasi. Hata kama ni kupitishwa tu kwamba imepitishwa lakini implementation iongoje Bunge lingine, itakuwa safi. Maanake tukona nini? Na nguzo. Lakini bila nguzo, kazi bure. Lakini hakuna makosa Rais sasa akivunja Bunge ni haki yake ki sheria.

**Elijah:** Ninafikiri mumesikia haya yote kutoka kwa Commissioner wetu, nafasi hii ninpea the Chairman wa Committee wetu wa hapa Baringo, apee Commissioner vote of thanks na tena pia kushumkuru kama Coordinator watu wote wa North Baringo kwa kuchangilia na kwa kutusikiliza na ninafikiri, Chairman atanimalizia. Chairman jaribu, kufuiisha.

**Chairman North Baringo:** Asante sana Bwana Coordinator, commissioner Lenaola, wana nchi wote, mimi ninatoa shukrani kabisa mbele yenu, hata mbeke ya Mungu kusaidia Katiba ifaulu. Tumefanya kazi kubwa sana. Ninampongeza Bwana Commissioner, ninapongeza watu wa North Baringo, walijitoa, wakati wa hearing wa kutowa maoni. Tulikuwa na Division, Kipsaram na Kabartonjo. Walijitokeza sana. Wale Commissioners wa kwanza walijionea, tulifanya kazi ya Katiba sana, tulimobilize, tulizunguka kuwaeleza yao Katiba ya Africa Katika Kenya. (In Kikalenjin).

Kwa hivyo Bwana Commissioner, Mimi ninatowa shukrani kwako, wale wa kwanza walitembelea sisi kwa watu wa maoni, na hawakuwa watu wa karimu kama wewe. You are very gentle man, umeongea maridadi, umeeleza kinaganaga na vile tunataka, na ile kitu inaitwa wazee wa mitaa, wote walikuwa wanasema tunataka wazee wa mitaa. Kwa hiyo ililinga na ile kabisa. Vile hata hawa watu walikuwa wanakaa bure (in kikalenjin) na umetueleza, asante kwa hiyo. Kwa hivyo mimi ninasema shukrani. Mimi nilikuwa Chief, nili kuwa Senior, ndiyo watu wakasema tubadillishe hiyo. Kwa hayo machache, mimi ninashukuru Coordinator Bwana Latangule, ametusaidia. Ninashukuru Committee wangu, hata unajua hii, wacha hawa Committee wasimame wana kamati, mkokaribu kweli? Ninashukuru hawa Committee kuna mama hukuona saa ile mama Mrs. Sengech.

